**CHADEMA** yadai kufanyiwa mchezo mchafu

UKURASA 2



**SPIKA** Tulia ataka vyombo vya habari kusema kweli

UKURASA 4

**MADAKTARI** bingwa wahofia kushuka ubora wa huduma

UKURASA 4



Nchimbi alipotumia ziara ya kikada mikoa sita, kunadi uchumi maendeleo

Ukurasa 14

Leo tunatimiza miaka sitini ya Muungano wetu

Si haba

BUFE

IJUMAA MEI 3, 2024 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Wananchi anzeni kutathmini wabunge wenu wanachofanya

Ukurasa 13

SAFARI YA HAKI ZA MFANYAKAZI NCHINI

**Kutoka timtimu alizofumua Kawawa wa TFL 1955, hadi anayosawazisha Samia**

• Mizizi ya SU, CSR, Baraza la Wafanyakazi, viwanda...

Na Peter Orwa

KATIKA kilele cha Siku ya Muungano Tanzania katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam onyesho la kumaliza tukio lilihusu gwaride la askari polisi wa kikoloni visiwani, namna walivyopata madhila.

Sinema hiyo haipishani sana na uhalisia wa yaliyowakuta watumishi Waafrika katika sehemu mbalimbali katika ajira ya kikoloni.

Inapotajwa sura hiyo, chimbuko lake ni karne ya 18, pale maendeleo hayo yalionekana sana katika nchi za barani Ulaya kama vile Ubelgiji, Uswisi na Uingereza kulikoibuka Mapinduzi ya Viwanda.

Ni hali iliyoibua bandari maarufu za Uingereza kama Derbyshire na Yorkshire, zikipokea malighafi kwa wingi kutoka nchi zilizotawaliwa, makoloni kama Tanzania yakawa vyanzo vya malighafi yanayoingizwa huko kupitia bandari hizo na nyingine maarufu.

Penye viwanda kukaibuka matabaka ya waajiriwa na waajiri, mabwanyenye wamiliki wa miradi ya viwanda. Msingi wake, wafanyakazi walionewa na kulalamika sana, hawakumiliki chochote, kasoro nguvukazi zao wakipewa maslahi na haki duni.

Ndicho kilichokuwapo upande wa wazalishaji, hasa penye makoloni kunakopatikana malighafi, pia wachache wanaotumikia serikali za kikoloni mahali hapo katika majukumu ya chini.

Rashid Kawawa; aliratibu mgomo wa wafanyakazi kitaifa, ikatikisa mno serikali ya koloni la Kiingereza wakati huo. **PICHA: MAKTABA.**

Hawakupata fursa za elimu, isipokuwa kwa wachache waliobahatika nao wengi hawakufika ngazi za mbali.

VUGUVUGU LA HAKI

Ni mazingira yaliyoanzisha fukuto la kudai haki kutoka viwandani, baadhi yao jamii ya watu weusi waliohamishiwa huko ughaibuni kudai haki zao kazini.

Ndio ukawa mwanzo wa kuzaliwa harakati za kudai haki za wafanyakazi, pia baadaye vyama vya haki za watendaji siasa za vyama vya wafanyakazi zikaanza, mfano hai nchini Uingereza.

Hiyo ikavuka ng'ambo ya pili, msukumo wa wafanyakazi ukaungwa mkono na wanaharakati wa haki za wanyonge, watetezi wa watu wa chini iliyojulikana kama Fabian Society, Uingereza.

Hatima yake ilipohamia kwenye siasa, ikazaa chama cha Labour, ambacho kiitikadi hadi sasa kiko mlengo wa kushoto kwa jamii ya watu wa chini au maarufu siasa za 'wastani' wakichuana na wenye itikadi za kulia uchumi huria 'wenye nacho wamiliki.'

KOLONI TANZANIA

Nchini Tanganyika wakati huo nao kukaguswa na hali hiyo, somo la Uingereza, hasa baada ya vita kuu vya dunia na kuzaliwa Umoja wa Mataifa (UNO sasa UN). Nyendo za madai ya haki za wafanyakazi zikachukua nafasi, sambamba na uhuru wa kujitawala.

Hadi kufika mwaka 1955, kilikuwapo kilichoitwa Tanganyikia Federation of Labour (TFL), chini ya Katibu Mkuu 'jembe', Rashid Mfaume Kawawa, aliyeratibu umoja na msukumo wa kundi kubwa la watendaji kazini, ikiwamo viwanda vichache, pia mashamba ya mkonge yaliyomea kitaifa wakati huo.

Ikizingatiwa Tanganyika ilikuwa koloni la mpito (non settler colony), Wajerumani na hata baadaye Waingereza, hapakuwapo uwekezaji wa kudumu, hivyo hawakuwekeza sana miundombinu na miradi, kama ilivyo Kenya na South Rhodesia (Zimbabwe).

Kundi kubwa la Watanganyika waliajiriwa mashambani panakozalishwa malighafi na wachache ofisi ya serikali wakitumikia ngazi ya chini.

Akiwa kijana wa miaka 29 mwanaharakati na mzalendo 'kupitiliza' anayetokea masomoni Tabora, Kawawa alifanya mageuzi makubwa ya kudai haki za wafanyakazi TFL, kati ya mwaka 1955 na 1956 kukashuhudiwa mgomo mkubwa dhidi ya watawala wa Kiingereza.

Kwa namna ya pekee migomo hiyo, chini ya uratibu wa 'jembe' Kawawa kitaifa ilitikisa Shirika la Reli Afrika Mashariki (EARC) chini ya (Balozi) Christopher Kassanga Tumbo na mwingine katika Kiwanda cha Bia, Dar es Salaam.

Inaendelea Uk 12

UKURASA 11

Ijumaa Mei 3, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581665

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

Maoni@nipashe.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Mjadala mzito bungeni mikopo kausha damu



**"Serikali lichukueni jambo hili kwa uzito unaostahili kwa sababu wananchi wanapata tabu." – Spika Tulia**



**"Mikopo unarejesha kila siku na siku moja ukivusha wanakuja na gari wanabeba kitanda na kila kitu... Watu wanajiua, serikali nendeni mkafanye utafiti." – Felista Njau**



**"Kuna kampuni zinatoa mikopo ya Sh. 100,000 na mkopaji anapaswa kulipa ndani ya siku mbili Sh. 150,000 na anaposhindwa anachukuliwa vitu vyake."- Sophia Mwakagenda.**



**"Kampuni za mikopo kupitia simu za mikononi zinatoa kwa riba ya asilimia 80 ndani ya siku saba anatakiwa kulipa na anapochelewa wanasambaza jina na picha za mkopaji kumdhalilisha." – Shally Raymond**

UKURASA 2



Wachimbaji wadogo katika Mgodi wa Mwakitolyo, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wakichenjua dhahabu kwa teknolojia ya kienyeji bila ya kuchukua tahadhari yoyote kwa kuvaa vifaa maalumu ili kujikinga na madhara ya kemikali ya zebaki, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

UKURASA WA 5

## 'TAKWIMU HURIA KUDUMISHA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI, KUTHAMINI USHIRIKIANO MAREKANI NA TANZANIA'

Toka mwaka 1993, kufuatia mapendekezo ya Mkutano Mkuu wa UNESCO, Siku ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari imekuwa ikiadhimishwa kote duniani kila tarehe 3 Mei. Mwaka huu, nimepewa ...

# Ongezeko wagonjwa afya ya akili lazidi kuwa tishio

UKURASA 3

## Mikoa saba kukumbwa kimbunga 'Hidaya'

UKURASA 3

**MICHEZO** MAJALIWA MGENI BETIKA TULIA MBEYA MARATHON UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# CHADEMA yadai kufanyiwa mchezo mchafu

**Na Francis Godwin**, IRINGA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimedai kuchafuliwa na mabango yenye picha za wanawake wa Baraza la Wanawake wa Chadema (BAWACHA) yaliyobandikwa kila wanapokwenda yanayotafsiri chama hicho na serikali hawana tatizo.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya Mwembetogwa, alisema mabango hayo makubwa yapo nchi nzima kwenye miji.

Lissu alisema mabango hayo yanatumika kuwachafua kwa wananchi kuonyesha CHADEMA na serikali hawana tatizo akifafanua kuwa, tatizo lipo ndio maana wana andamana.

"Mabango haya yanatumika kuchafua kwa wananchi kuwa sisi na serikali hatuna tatizo, ama kuonyesha tumehongwa, ila ukweli mabango haya hata sijui kwa nini tulimualika ila haina shida, ukweli CHADEMA tunaandamana kwa kuwa, tunaona shida ipo kubwa, tunaandamana kudai Katiba mpya," alisema.

John Heche, alisema CHADEMA inaomba Watanzania wote kuunga mkono maandamano hayo, kwa kuwa hivi sasa chama hicho kinaugulia maumivu kwa kukimbiwa na wenyeviti wa serikali za mitaa pamoja na wabunge na madiwani ambao kwa maelezo yake, walinunuliwa na serikali ya CCM.

Alidai kuwa, serikali ya awamu ya tano iliacha maumivu makubwa ndani ya CHADEMA kwa kuwanunua wenyeviti na madiwani wake.

Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Iringa Mjini, Frank Nyalusi, alisema wamezuiwa kutumia njia ya Kihesa na kuruhusiwa njia moja pekee ya Mlandege hadi viwanja vya Mwembetogwa.

"Maandamano haya ni mwanzo wa maandamano na mkutano mkubwa wa CHADEMA Mkoa wa Iringa ambao utafanyika katika viwanja Mwembetogwa na kuwa maandalizi ya maandamano hayo ni ya siku moja pekee, ndiyo sababu ya watu kutokuwa wengi, lakini jambo kubwa ni kufikisha ujumbe serikalini kuhusu hitaji la msingi la kudai Katiba mpya," alisema.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa, alisema sababu kubwa ya kuandamana ni kudai Katiba mpya pamoja na kuiambia serikali kuhusu ugumu wa maisha kwa Watanzania.

"Kuna baadhi ya watu wanabeza maandamano ya CHADEMA kwa kuona hayawahusu, ila nao ni miongoni mwa watu wanaokosa haki kutokana na katiba mbovu na pia, wanalia ugumu wa maisha kwa kuendelea kushuhudia gharama za bidhaa zikiendelea kupaa siku hadi siku.

"Naomba kuwaambia Watanzania, maandamano haya si ya CHADEMA pekee, ni ya watanzania wote, maana Katiba mpya si ya CHADEMA ni ya taifa zima," alisema.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya Wabunge kwenye kipindi cha maswalı kwake Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mjadala mzito mikopo kausha damu bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIKOPO ya 'kausha damu' imeibua mjadala mzito bungeni huku Bunge likitoa miezi mitano kwa serikali kufanya tathmini ya kina ili kupata namna ya kushughulikia suala hilo lisilete athari kubwa kwa wananchi.

Mjadala huo uliibuka jana baada ya kipindi cha maswali na majibu na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitaka serikali itoe majibu ya mikopo hiyo iliyoibuliwa na wabunge hivi karibuni, wakiwamo Felista Njau (Viti Maalum-CHADEMA) na Shally Raymond (Viti Maalum- CCM).

Wabunge hao walisema mikopo hiyo inatolewa na taasisi za fedha zenye leseni na baadhi ya kampuni za simu hali inayowaumiza wananchi na wengine kufikia hatua ya kujiua.

Akizungumzia suala hilo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema kwa mujibu wa Sheria za Fedha zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) hakuna kampuni ya simu iliyopewa leseni ya kutoa mikopo kwa wananchi.

Alisema kampuni zinatoa huduma za fedha kwa kutumia leseni za kutoa huduma za mifumo ya malipo kwa matakwa ya sheria ya fedha na kanuni zake.

"Mikopo inayotolewa kwa wananchi kupitia simu ni kati ya taasisi zilizopewa leseni ya kutoa mikopo pamoja na kampuni za simu," alisema.

Alisema BoT imekuwa ikitoa elimu ya huduma za kifedha ili kujiepusha wananchi kuchukua mikopo kwa watu wasio na leseni kutoka benki hiyo.

"Mikopo iliyopata umaarufu kuitwa kausha damu hutolewa na taasisi zisizo na leseni kutoka Benki Kuu, Benki Kuu ilishaelekeza kampuni za simu kuhakikisha mifumo yake haitumiki katika mikopo hiyo na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kutochukua mikopo kwa kampuni ambazo hazijasajiliwa na hazina leseni za kutoa mikopo,"alisema.

Alisema BoT inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua kwa wale wanaokiuka taratibu zilizowekwa na kusisitiza hakuna kampuni ya simu inayotoa mikopo bali ni taasisi za fedha zinatoa mikopo kupitia mifumo ya kampuni za simu.

Alisema utaratibu wa sheria za kifedha una mwongozo ambao hautoi fursa ya mtu kufanya suala la utoaji mikopo kiholela.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa kanuni ya kuwalinda walaji taasisi za fedha zote wigo wa juu hawatakiwi kuzidi riba ya asilimia 3.5 kwenye mkopo wa mwezi mmoja.

Naye, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema mitandao ya simu haichukui leseni ya kutoa mikopo isipokuwa wao wanaingia mkataba wa uwezeshaji wa kutoa huduma na mtoa huduma mwenye leseni ya BoT.

"Wizara yangu tuliwaagiza TCRA wakapitie kampuni za simu ziangalie taasisi zinazofanya nazo kazi zenye leseni BoT, upande wa serikali tumechukua hatua na tunaendelea kuelimisha watu, mimi nadhani pamoja na jambo hili kulifanyia kazi lakini wananchi wasiparamie mikopo hii ambayo haina kichwa wala miguu, ni rahisi kuipata lakini ina gharama,"alisema.

Kutokana na majibu ya Mawaziri hao, hali hiyo ilimlazimu Spika Tulia kuruhusu wabunge kuchangia mjadala wake ndipo Njau aliposema imeathiri wananchi na kuna taasisi zina ofisi na zinatoza riba ya asilimia 60 hadi 80 kwenye mkopo.

"Mikopo unarejesha kila siku na siku moja ukivusha wanakuja na gari wanabeba kitanda na kila kitu. Nataka kujua hii mikopo riba yao mwisho asilimia ngapi maana mwongozo wa BoT upo lakini haufuatwi.

Watu wanajiua, serikali nendeni mkafanye utafiti mfuatilie, "alisema.

Mbunge Shally alisema kuna kampuni za mikopo kupitia simu za mikononi zinatoa kwa riba ya asilimia 80 ndani ya siku saba anatakiwa kulipa na anapochelewa wanasambaza jina na picha za mkopaji kumdhalilisha.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, alisema: "Mawaziri hawajaelewa adha wanayopata wananchi hasa wanawake. Kuna kampuni zinatoa mikopo ya Sh. 100,000 na mkopaji anapaswa kulipa ndani ya siku mbili Sh. 150,000 na anaposhindwa anachukuliwa vitu vyake. Naomba serikali ilichukue suala hili wakalifanyie kazi."

Mbunge wa Manyoni Magharibi (CCM), Yahaya Masare alisema watu wanakopeshwa fedha kidogo lakini riba kubwa na ulipaji wake ni wa muda mfupi, hivyo serikali inapaswa kuliona hilo.

Akihitimisha hoja hiyo, Spika Tulia alisema kutokana na majibu ya serikali, bunge linashindwa kutoa maazimio, hivyo kutoa muda zaidi wa suala hilo kufanyiwa kazi kwa kuwa linaumiza wananchi.

"Hii hoja ya mikopo yenye riba kubwa sana si hoja tu ya wale wanaotoa mikopo kwa urafiki au kwa kujuana. Taasisi za kifedha zinadai riba kubwa hata zenye leseni na kwa kuwa leseni zinatolewa na serikali hili ndilo jambo la kwenda kutazama.

"Kama taasisi iliyosajiliwa inaweza kutoza riba hadi asilimia 80, yule wa kijijini atafanya hivyo na hata wa simu. Kwa wale wenye leseni serikali mna uwezo wa kuwafuatilia na hilo tusiwasukumie wananchi kwamba wanakimbilia kwa sababu hawana namna nyingine.

"Serikali lichukueni jambo hili kwa uzito unaostahili kwa sababu wananchi wanapata tabu. Sasa katika hoja hii kwa namna mjadala ulivyokuwa, ni ngumu kusema Bunge linaazimia nini kwa kuwa ni pana tofauti na ilivyofikiriwa mwanzo pengine ni kundi fulani, kumbe taasisi zenye leseni zinatoa riba kubwa,"alisema.

Spika alitaka serikali ifanyie kazi suala hilo kwa kufanya tathmini na kutoa mwongozo utakaopunguza riba na kuondoa tabu wanazopata wananchi.

"Kwa kuwa jambo hili ni pana serikali inahitaji muda wa kutathmini kuangalia hali halisi na kutoa mwongozo. Naamini katika kipindi hiki cha bunge watumie muda mrefu kuwasikiliza wabunge na wananchi kwa kweli athari ni kubwa sana na tutasikia Bunge la mwezi wa tisa kama wamepiga hatua yoyote lakini kwa maana ya majibu lazima wafanye utafiti," alisema.

# Mikoa saba kukumbwa kimbunga 'Hidaya'

**Na Faustine Feliciane**

MIKOA saba nchini inatarajiwa kuathirika na kimbunga 'Hidaya' kilichotarajiwa kusogea pwani ya Tanzania kuanzia usiku wa kuamkia leo.

Mikoa inayotarajiwa kupata athari ya mvua kubwa kutokana na kimbunga hicho ni Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Tanga, Pwani, Pemba, Unguja na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) iliyotolewa jana, mgandamizo mdogo wa hewa umezidi kuimarika zaidi na mpaka kufikia jana tayari kimbunga Hidaya kilikuwa kilomita 506 kutoka Pwani ya Mkoa wa Mtwara.

"Jana (juzi) tulitoa taarifa ya kuwapo kwa mgandamizo mdogo wa hali ya hewa karibu na pwani ya mkoa wa Mtwara, mgandamizo huo imezidi kuimarika na kutengeneza kimbunga Hidaya ambapo kinatarajiwa kufika kwenye Pwani ya nchi yetu usiku wa kuamkia kesho (leo)," ilisema taarifa ya jana ya TMA.

Hali hiyo ya kuwapo kwa kimbunga Hidaya kutasababisha upepo mkali na mvua kubwa hususani leo kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara na kusambaa kwenye maeneo mengine ya pwani ya Tanzania kufikia kesho.

"Wananchi wote wanaofanya shughuli zao baharini wanashauriwa kuchukua tahadhari na pia kufuatilia taarifa za tahadhari kutoka TMA," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, Mamlaka hiyo imewataka wananchi kufanyia kazi ushauri wa kitaalam kutoka kwa sekta husika kuhusu athari hizo.

Hali ya kimbunga na mvua kubwa kunatarajiwa kuanza kupungua Mei 6, mwaka huu.

Taarifa hiyo ya TMA imekuja huku baadhi ya maeneo ya nchi yakiendelea kukumbana na athari ya mvua kubwa inayoendelea kunyesha nchini.

Baadhi ya mikoa mbalimbali hapa nchini imeathirika na mvua ikiwamo mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Zanzibar na kuharibu miundombinu na makazi ya watu.




Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakigombea kupanda kwenye basi la mwendokasi kwa kupitia upande usio rasmi kwa kupakia abiria kutokana na shida ya usafiri huo, katika eneo la Kimara Temboni, Barabara ya Morogoro, jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Ongezeko wagonjwa afya ya akili lazidi kuwa tishio

**Na Pilly Kigome**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Sarea, amesema kumekuwa na ongezeko la magonjwa ya afya ya akili na kwamba kwa wiki wanapokea wagonjwa 20 hadi 30 wakiwa katika hatua ya mwisho ya kuugua.

Amesema awali walikuwa wanapokea wagonjwa chini ya 10 kwa siku.

Dk. Sarea aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akitoa tathmini ya utafiti mkubwa wa pili uliofanyika kati ya Tanzania na Ghana na kushirikisha nchi 13.

Alisema katika sensa yao ya mwaka 2022/23, wanaougua magonjwa hayo, asilimia 19 ni vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24.

Dk. Sarea alitaja kichochea kikubwa cha ongezeko hilo kuwa ni kipindi cha mwanamke anapobeba ujauzito bila utayari kwa kipindi hicho.

"Pia namna anavyopewa huduma za umuhimu na mwenza wake na familia kwa ujumla ikiwamo na mabadiliko ya uchumi na kijamii, huongezeka mtikisiko wa tatizo hili.

"Unyogovu, wasiwasi, matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo na kuiga tamaduni zisizo za kitanzania na ongezeko la utandawazi kwa kiwango kikubwa hizi zote ndio visababishi la ongezeko la magonjwa hayo," alisema.

Dk. Sarea alisema kutokana na ongezeko hilo, wanapokea takribani wagonjwa 20 hadi 30 kwa wiki hospitalini hapo ambao tayari wako katika hatua za mwisho za kuugua magonjwa hayo.

Mtaalamu huyo alisema sababu nyingine zinaanzia kwa familia pindi mtoto anapozaliwa na malezi yake katika ukuaji.

"Mtoto anaishi na nani katika malezi ya ukuaji wake, anasimamiwa na nani mambo yake ya karibu ikiwamo elimu, changamoto za mtoto zinatatuliwa vipi katika maisha yake ya kila siku, makuzi na mambo mengine yahusuyo mtoto," alibainisha.

Dk. Sarea alitaja sababu ndogondogo za kugundua viashiria vya ugonjwa afya ya akili kwa makundi yote, ikiwamo na kukosa usingizi, utumiaji wa kilevi kupitiliza, kuongea mwenyewe.

Kuhusu yanayopaswa kufanyika, mtaalam huyo alisema ni familia na jamii waanze kumwangalia kwa ukaribu mjamzito, kuwekeza katika malezi ya mtoto na wazazi waangaliwe afya zao za akili kama ziko sawasawa. Pia aliitaka jamii ipewe elimu kuhusiana na afya ya akili, kwani sababu hizo waweza kuwa ni mwarobaini wa kuondokana na tatizo hilo linalowakabili vijana.

Mtafiti Mwandamizi na Mratibu wa Mradi huo mkubwa wa pili uliofanyika Tanzania na Ghana kuhusiana na magonjwa ya akili, Dk. Innocent Yusuf, alisema utafiti umefanyika katika nchi 13 za Afrika, Asia na Ulaya.

Alisema umeibua mambo mbalimbali yaliyobaini waathirika ni kundi la vijana na unyanyapaa kwa wale wenye tatizo la afya ya akili wanaopitia changamoto mbalimbali akitolea mfano wenye maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU).

"Changamoto za maisha katika familia yake kutikisika kiuchumi zinaweza kusababisha kijana kupata mawazo, kupatwa na msongo wa mawazo uliopindukia na kupelekea kuathiri afya yake ya akili.

"Sababu nyingine kubwa ni mazingira ya malezi kumekuwa na mabadiliko ya malezi, ongezeko la utandawazi na kuchukua tamaduni ambazo si za kitanzania," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali Afrika Academy Public Helth (AAPH), Dk. Mary Mwanyika, alisema utafiti umeonyesha kuelekea kupoteza kundi la vijana, kwa kuwa wengi wao wana dhana ya kujinyonga kutokana na changamoto hizo.

Dk. Mwanyika pia alisema uelewa mdogo katika jamii, upatikanaji mdogo wa huduma za afya ya akili ni mkubwa kutokana na imani za kitamaduni zenye nguvu kwa kuenea kwa fikra potofu.

"Asilimia kubwa ya jamii ina dhana kwamba, watu wenye matatizo ya afya ya akili ni ushirikina na wanahitaji kutibiwa kwa waganga wa jadi. Hii inajitokeza zaidi katika maeneo ya vijijini ambapo imani na mila nyingi za jadi bado zipo kwa kiasi kikubwa," alisema.


**ABBOTT FUND TANZANIA**

**(NGO Certificate of Registration Number 00483)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON-GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT (AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations requires that all non-governmental organisations in Tanzania publish biannually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE**, we wish to make the following public disclosure of the funds approved for 2023 activities and their expenditure, which publication covers the reporting period from **1st July 2023 to 31st December 2023:**

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Leadership Capacity-Building. | 126,000 |
| **Emergency Medicine Regional and District Amplification:** Includes support to MNH Emergency Medicine, and EMD infrastructure project. | 550,000 |
| **Village Emergency Care Model** in Dodoma, Mbeya and Tanga. | 434,000 |
| **Building Livelihoods**: Includes support to National Children's Centre in Dodoma. | 290,000 |
| **Mapatano Project:** Includes infrastructure project at Mapatano Secondary School. | 2,110,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff. | 1,932,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2023.** | **5,442,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA**




Daktari Bingwa wa Macho kutoka Hospitali ya Rufani ya mkoa wa Pwani-Tumbi, Matthew Yinza (kulia), akimfanyia uchunguzi wa macho mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule ya msingi Mwambisi, Niraf Hamadi, kwa msaada wa shirika lisilo la kiserikali la Vision Care kutoka Korea Kusini, katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, mkoani Pwani jana. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

# Spika ataka vyombo vya habari kukosoa badala kusifia kila kitu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema licha ya serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, vyombo vya habari havipaswi kujenga utamaduni wa kusifia kila kitu bali vikosoe pale kunapokuwapo na matatizo ili yafanyiwe kazi.

Dk. Tulia alisema hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua maadhimisho ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani.

"Pale ambapo tumefanya vizuri mtusifie lakini chombo cha habari si kusifia tu kila kitu.

Hata kama tutakuwa tumejenga kituo cha afya lakini hakuna wataalamu au dawa tuambiwe ili tufanyie kazi yale ambayo bado ni changamoto kwa wananchi wetu," alisema.

Pia alisema vyombo vya habari nchini ni lazima vijengewe uwezo kiuchumi ili kuwa na nguvu ya kutoa habari bila kumtegemea mtoa habari.

Alisema wakati huu ambapo taifa linaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, atashirikiana na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhakikisha vyombo vya habari vinalipwa madai yao katika taasisi mbalimbali za serikali.

"Awali Waziri ulisema vyombo vya habari vinapaswa kutenda haki kwenye uchaguzi lakini pia ukasema uchumi wa vyombo vya habari ni shida, hivyo wasiwasi wangu ni kwamba kuna watu ambao wanakuwa na vyombo vya habari na wanavilipa wenyewe. Hii inaweza kuwa moja ya sababu za kutokuwa na usawa," alisema.

Spika Tulia alisema kutokana na hali hiyo, atasimamia madeni yote ambayo taasisi zote za serikali zinadaiwa na vyombo vya habari ili kuviwezesha kujiimarisha kiuchumi ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara ya wafanyakazi wao.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, alisema kutokana na utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kumekuwapo na mabadiliko makubwa kwenye uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Alisema pamoja na kuwepo kwa uhuru wa vyombo vya Habari, shida bado iko kwenye uchumi wa vyombo vya Habari na vingi vina hali mbaya kifedha.

"Mweshimiwa mgeni rasmi, pamoja na hatua kubwa ambazo tumepiga ikiwamo kupunguza fungafunga ya vyombo vya Habari, changamoto bado kwenye uchumi wa vyombo vya Habari. Vingi vinafungwa kutokana na hali mbaya kiuchumi," alisema.

Alisema vyombo vingi vinaidai serikali kiasi kikubwa cha fedha ambacho kama kitalipwa, kitasaidia kupunguza ugumu wa maisha uliopo hivi sasa.

Kadhalika, Nape alitoa rai kwa vyombo vya habari kutoa haki sawa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu kwa wagombea bila kujali vyama vyao au hali zao.

Rais wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Deogratius Nsokolo, alisema wanaishukuru serikali kwa kufanyia marekebisho baadhi ya vifungu vilivyokuwa kikwazo kwa waandishi katika Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kufanya marekebisho ya vifungu tisa ambavyo vilikuwa kikwazo kwenye sheria ya huduma ya habari na nimatarajio yetu kuwa sheria zingine ambazo bado ni kikwazo kwetu zitafanyiwa marekebisho ili kutupa uhuru wa kutekeleza majukumj yetu," alisema Nsokolo.

# Tani milioni 1.15 nafaka kuimarisha usalama wa chakula

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KATIKA kuhakikisha nchi inakuwa na utoshelevu wa chakula, serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeeleza mpango wake wa kununua tani milioni 1.15 za nafaka ili kuimarisha usalama wa chakula.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo bungeni jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2024/25.

Bashe alisema wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) katika mwaka 2024/25 itanunua tani 1,150,000 za nafaka ili kutimiza lengo hilo.

Pia alisema NFRA itaendelea kuuza chakula kwa maombi maalumu na kutoa chakula cha misaada pale itakapohitajika katika nchi za jirani na nje ya ukanda wa Afrika.

Kadhalika, alisema wizara kupitia NFRA itakamilisha majadiliano na Benki ya NBC kuanzisha Hati Fungani ya Usalama wa Chakula ili kuongeza uwezo wa NFRA kuhifadhi chakula.

**BBT NA AJIRA**

Kuhusu upatikanaji ajira, Waziri Bashe alisema wizara inaongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo na itaendelea kuongeza fursa hizo kupitia utekelezaji wa Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) inayotekelezwa kupitia miradi mikuu minne.

Alisema program hiyo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja na umilikishaji wa ardhi, kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa vijana na wanawake (BBT - Mitaji), kuimarisha Huduma za Ugani (BBT - Ugani) na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT -Visima).

Hatua hiyo, alisema itafikiwa kupitia utekelezaji wa mradi wa mashamba makubwa ya Chinangali, Chunya, Singida na Ndogowe kwa kujenga mabwawa na kuchimba visima kwenye mashamba ya BBT jumla ya hekta 186,086.

**HALMASHAURI KUNUFAIKA**

Waziri Bashe alisema wizara itaanza kutekeleza mradi wa BBT katika halmashauri 100 zitakazotenga maeneo yenye ukubwa wa hekta 200 kwa kila moja na kujenga miundombinu ya umwagiliaji.

"Utambuzi wa vijana watakaomilikishwa ardhi utafanywa na halmashauri husika ambapo Wizara ya Kilimo itatoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana hao katika maeneo yao," alisema.

Pia alisema serikali kupitia AGITF itaongeza mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake waliopo kwenye shughuli za kilimo na uongezaji thamani mazao kutoka Sh. bilioni mbili mwaka 2023/24 hadi Sh. bilioni 10.

# Madaktari bingwa wahofia kushuka ubora wa huduma

**Gwamaka Alipipi na Restusta James**

MADAKTARI bingwa wa magonjwa ya ndani, wameelezea hofu y kushuka kwa huduma iwapo baadhi ya mambo hayatarekebishwa.

Maeneo mawili waliyotaja ya kuboresha ili kuimarisha huduma za afya ni Pamoja na uwekezaji kwenye huduma za kimaabara ambazo zimekuwa hafifu.

Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA), Dk. Mwanaada Kilima, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho.

Dk. Kilima alisema licha ya serikali kuboresha huduma za afya nchini kwa kujenga vituo vya kutolea huduma, bado kuna upungufu wa watumishi na baadhi ya huduma za maabara kubwa (sampuli) zinapelekwa nje ya nchi.

"Kwa mfano kwenye mwongozo wa taifa wa matibabu kuna vitu vinapaswa kubadilika. Tulipeleka maoni yetu kupitia Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kuhusu nini kifanyike katika vitita vipya vya matibabu. Hali ikiendelea hivi ubora wa matibabu utashuka na sisi hatupendi itokee hivyo," alisema.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akifungua mkutano huo, alisema ni kweli kwenye huduma za kimaabara serikali haijafanya vizuri katika uwekezaji.

Alisema kupitia mpango uitwao Samia Scholarship wa mwaka 2023/24, serikali ilitumia Sh. bilioni 10.9 kuwasomesha wanafunzi wakiwamo madaktari bingwa 79 wa magonjwa ya ndani.

Kuhusu bima ya afya, Waziri Ummy alisema asilimia nane ya Watanzania ndio wanaotumia huduma hiyo kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ma asilimia 0.5 wanatumia bima ya afya binafsi.

"Leteni mapendekezo yenu mtusaidie namna ya kuboresha kitita cha bima ya afya hususani katika dawa, tiba. Sasa hivi kuna ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza kama vile figo, hivyo tunawategemea sana nyie (madaktari) mtusaidie namna ya kuzuia tatizo hili," alisema Ummy.

Alisema kunapaswa kuwa na mwongozo wa taifa wa matibabu katika matumizi ya bima ya afya, hivyo aliwaomba madaktari hao kupeleka maoni ya namna bora ya kuboresha. Waziri Ummy alisema mipango ya serikali ni kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini, ikiwemo kuhakikisha hospitali zote za rufaa za mikoa kuwa na uwezo wa kutoa huduma za kibingwa katika huduma za fani nane.

Alizitaja huduma hizo ni afya ya uzazi na mama, watoto, magonjwa ya ndani, upasuaji, huduma za dawa za usingizi na ganzi, radiolojia, upasuaji mifupa na dharura na ajali. "Hadi sasa, hospitali za rufaa za mikoa nane ndio zina uwezo wa kutoa huduma kwenye fani zote nane na hivyo kazi bado inaendelea ili kuziwezesha hospitali zote 28 kutoa huduma za kibingwa," alisema Ummy.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Dk. Elisha Osati, alisema kwa sasa sekta ya afya ikabiliwa na tatizo la uhaba wa wataalamu maeneo ya vijijini, kwamba wataalamu wengi wanapatikana mijini.

Alisema serikali inapaswa kuweka nguvu katika kuboresha maslahi ya madaktari ili waweze kufanya kazi sehemu yoyote. Alisema kinachosababisha madaktari kukimbilia mijini ni upatikanaji wa maslahi.

HABARI KITAIFA

# ‘Takwimu Huria Kudumisha Uhuru wa Vyombo vya Habari, Kuthamini Ushirikiano Marekani na Tanzania’



Na Balozi Michael Battle

TOKA mwaka 1993, kufuatia mapendekezo ya Mkutano Mkuu wa UNESCO, Siku ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari imekuwa ikiadhimishwa kote duniani kila tarehe 3 Mei. Mwaka huu, nimepewa heshima kubwa kushiriki katika maadhimisho rasmi jijini Dodoma nikijumuika pamoja na maafisa wa serikali, wabia wa kimataifa, na viongozi wa asasi za kiraia.

Maadhimisho haya yanaangazia nafasi muhimu ya uhuru wa vyombo vya habari katika kukuza demokrasia imara kwa kuwezesha wananchi kufanya maamuzi yatokanayo na wao kuwa na taarifa sahihi na kuzifanya serikali na viongozi wake kuwajibika kwa umma.

Nchini Marekani, tunawathamini sana raia wenye taarifa sahihi na za kutosha kama msingi wa demokrasia.

Ni kwa sababu hiyo uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari vimelindwa kikamilifu katika Marekebisho ya Kwanza (First Amendment) ya Katiba ya Marekani.

Kipindi changu kama Balozi wa Marekani nchini Tanzania kimeimarishwa na kuboreshwa sana kwa kushirikiana na waandishi wa habari wa ngazi na aina zote. Raia wanaoandika au kupasha habari (citizen journalists) wakiwa na nafasi ya kipekee ya kuyaona mambo kwa namna tofauti na watu wengine, wanaweza kubadilisha mwelekeo wa taifa, na weledi wa waandishi wa habari waliofunzwa unabaki muhimu kwa kutoa muktadha na mwelekeo sahihi wa mjadala wa kitaifa.

Kwa pamoja, kazi yao inaonyesha wazi jinsi vyombo vya habari huria vinavyopambana na ujinga - adui mkubwa kati ya maadui watatu walioainishwa na Mwalimu Julius Nyerere - na hivyo kujengea uwezo jamii.

Hata hivyo, nguvu ya taarifa hutegemea ubora wa takwimu zinazounda taarifa hiyo.

Katika Siku hii ya Kimataifa ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, napenda kuangazia kazi bora ya taasisi iitwayo AidData, Taasisi ya utafiti wa takwimu iliyoko katika Chuo cha William & Mary nchini Marekani, ambayo leo imezindua ripoti inayotathmini thamani ya ushirikiano kati ya Marekani na Tanzania kwa watu wa Tanzania.

Marekani inashirikiana kwa kiwango kikubwa na Tanzania, ikiunga mkono na kusaidia miradi mbalimbali kuanzia miradi ya afya na kuwajengea watendaji uwezo (capacity building) hadi miradi ya kuimarisha utawala wa kidemokrasia.

Hata hivyo, ili kuelewa vyema thamani ya ushirikiano huo, ni muhimu kuwa na takwimu zinazoweza kupatikana na kutumiwa kwa urahisi.

Dhamira ya AidData ya kuongeza uwazi wa katika utoaji na usimamizi wa fedha za maendeleo ni muhimu sana.

Kwa kutoa takwimu za kina na zinazopatikana kwa urahisi kuhusu jinsi na wapi fedha za msaada zinatengwa na kuelekezwa, AidData inawezesha vyombo vya habari na umma kuziwajibisha serikali na taasisi za kimataifa kwa ufanisi.

Raia wote wanapaswa kuweza kuzifikia na kuzitumia takwimu huria kama njia ya kupima ufanisi na matokeo ya uwekezaji katika jamii zao.

Ripoti ya AidData inaonyesha kuwa Marekani, kupitia idara na taasisi za kiserikali, mashirika na watu binafsi, inachangia takriban Dola za Kimarekani bilioni 2.8 kila mwaka (takriban Shilingi za Kitanzania bilioni 7,140) kwa maendeleo ya Tanzania.

Aidha, tumefungua milango yetu kwa Watanzania kuishi, kufanya kazi, na kusoma nchini Marekani. Hali kadhalika, Kila mwaka, Watanzania waishio nchini Marekani (Tanzanian Diaspora) wamekuwa wakichangia dola milioni 96.4 za ziada katika uchumi wa Tanzania kupitia pesa zinazotumwa nchini kutoka Marekani.

Kwa miaka 20 iliyopita,ikiwa mfadhili mkubwa zaidi wa miradi ya kudhibiti maambukizi na matibabu ya VVU/UKIMWI, Marekani imezuia vifo vya mapema vya Watanzania wapatao takriban 750,000.

Kwa kupata takwimu huria, AidData imefanya kazi kubwa ya kupima matokeo ya ushirikiano kati ya Marekani na Tanzania kwa Watanzania wote.

Takwimu hizi zinatoa simulizi ambayo inawawezesha watu wa Tanzania kufanya maamuzi yatokanayo na taarifa sahihi kuhusu jinsi bora ya kushirikiana na mataifa washirika ili kufikia malengo yao ya maendeleo kitaifa.

Natumai kila mmoja atachukua muda kusoma ripoti hii na kutathmini yeye mwenyewe jinsi ushirikiano kati ya Marekani na Tanzania unavyogusa maisha yake ya kila siku.

Wakati wa ziara ya Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan alisema “Tunajitahidi kujenga taifa la kidemokrasia linalozingatia uwazi na kuheshimu utawala wa sheria.”

Tunaunga mkono maono haya ya Rais na tutaendelea kufanya kazi kwa bidii pamoja na Watanzania katika serikali na asasi za kiraia ili kuyafanya maono hayo kuwa hali halisi kwa Watanzania wote.

Leo, ninaungana na Wamarekani, Watanzania, na watu kote duniani, tunapotetea uhuru wa vyombo vya habari na kuunga mkono wananchi kupewa taarifa sahihi na toshelevu.

Kwani hakuna uhuru katika jamii bila vyombo vya habari huru, na tunailinda haki hiyo adhimu leo na kila siku.

# Watoa huduma za mawasiliano wapanda viwango

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema watoa huduma watano wa mawasiliano ya simu za mkononi, wamefikia viwango vilivyowekwa kwenye kanuni na kuvipita katika baadhi ya maeneo.

Hayo yamo katika rpoti ya utafiti wa hivi karibuni inayoonyesha ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini kwa robo mwaka inayoishia Machi, 2024 iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari.

Alisema ripoti hiyo inaonyesha matukio majaribio ya ulaghai na uhalifu kupitia simu za mkononi yamepungua kati ya Desemba, 2023 na Machi mwaka huu, kwa mujibu wa ripoti ya utafiti uliofanywa kwenye maeneo 15 ya utendaji wa watoa huduma za simu za mkononi Tanzania.

Dk. Bakari alisema watoa huduma wote wanakidhi vigezo vya ubora vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Ubora za Mwaka 2018 na kwamba TCRA ilifanya durusi ya ubora wa huduma kwenye maeneo 14 yanayohusu mitandao na eneo moja la usalama kati ya Januari na Machi 2024.

Aliwataja watoa huduma hao kuwa ni Airtel, Halotel, Tigo, TTCL na Vodacom na kwamba durusi ilihusisha upatikanaji wa mitandao kwa watumiaji wanaotaka kupiga simu, idadi ya simu ambazo zinashindikana kuunganishwa mitandaoni kwa sababu za kiufundi na zile zinazokatika katikati ya maongezi.

TCRA pia ilifuatilia kuenea kwa teknolojia ya simu za mkononi za uzao wa pili, tatu na nne, yaani 2G, 3G na 4G pamoja na uzao wa pili unawezesha maongezi na meseji, wa tatu na wa nne inawezesha vyote hivi na pia matumizi ya data, hasa kwa huduma intaneti.

“Kuenea huduma za 3G miongoni mwa watu kuliongezeka kutoka asilimia 86 hadi 88 na 4G kutoka asilimia 79 hadi 80. Kuenea kwa uzao wa 5 ni asilimia 13,” alisema.

Alisema mengine kwenye durusi hiyo ni ufanisi wa kufikisha simu kwenye minara na ubora wa simu kwa watumiaji wanapokuwa wanatembea na kwamba TCRA pia ilipima kasi ya kusafirisha data kwenye mitandao, na hadi kufikia vifaa vya watumiaji.

“Ufuatiliaji wa ulaghai na uhalifu kwa njia ya simu za mkononi umeonesha kuwa matukio yamepungua kwa asilimia 17 kati ya Desemba 2023 na Machi 2024 - kutoka 20,939 hadi 17,318,” alisema.

Pia alisema mikoa ya Morogoro na Rukwa inaongoza kwa matukio zaidi yaliyoripotiwa, ikiwa na zaidi ya theluthi moja ya matukio nchini.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, matukio mikoa ya Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na mikoa yote ya Pemba ni kati ya matatu na mawili; hali ni tofauti kwa Mkoa wa Mjini Magharibi, ambao ni wa 20 kwa nchi nzima, ukiwa na matukio 33.

Aidha, ripoti inataja watoa huduma waliokumbwa na ongezeko la matukio. Yaliongezeka kwa asilimia 30 kwenye mtandao wa Vodacom - kutoka 2,876 robo mwaka iliyoishia Desemba 2023 hadi 3,735 Machi 2024.

Uchambuzi wa matukio na idadi ya laini za kila mtandao unaonesha idadi ya matukio ya Vodacom ni chini ya TIGO, ambayo pamoja ja kupunguza kwa asilimia 26 bado ina 6,011. Airtel ilipunguza matukio wa asilimia 21 lakini bado inayo 5,120.

Halotel ina 148 - ambayo ni chini kuliko mitandao yote. TTCL ina 2,304.

Ikilinganishwa kwa idadi ya laini zilizosajiliwa kila mtandao, Tigo, yenye laini 20,300,45, ina uwiano wa juu zaidi - 0.29. Uwiano kwa watoa huduma wengine na idadi ya laini za mitandao hiyo kwenye mabano ni TTCL, 0.14 (1,676,541), Airtel,0.02 (19,465,353), Vodacom, 0.017 (22,629,341) na Halotel, 0.002 (9,354,092).

Dk. Bakari aliwataka watumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu, wamekuwa wakichukuwa juhudi za ziada kwa kutoa taarifa ya namba za simu jinazotumika kwenye Ulaghai na Utapeli kwa kutuma namba hizo kwa Ujumbe mfupi kwenda 15040, bure.




Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Kagera na Mkurugenzi wa shirika la Omuka Hub, Neema Lugangira, akitoa mada kwenye kongamano la maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari Duniani, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la Nukta Afrika, Nuzlack Dausen. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mazoezi, ulaji unaofaa utapunguza magonjwa haya

**MAGONJWA** yasiyo yakuambukiza yanaelezwa kusumbua watu wengi hasa wenye umri mkubwa kutokana na kutozingatia vizuri mtindo wa maisha yao.

Magonjwa yasiyoambukiza ni yale ambayo hayasambazwi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa kuwa hayana vimelea vinavyohusiana na magonjwa hayo.

Katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwa mojawapo ajali za barabarani na madhara yatokanayo na vilevi yamewekwa kwenye orodha ya magonjwa yasiyoambukizwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), magonjwa yasiyoambukiza ndio yanayoongoza kwa kusababisha vifo duniani.

Utafiti unasema asilimia 72.8 duniani ya vifo vinasababishwa na magonjwa yasiyoambukiza na shinikizo la damu limekuwa kichocheo kikubwa.

Utafiti huo uliofanywa na Nature mwaka 2007 umeripoti kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanaua kwa kasi zaidi kulinganisha na yale yanayoambukiza.

Kutokana na takwimu hizo za kidunia kwa hapa nchini katika utafiti uliofanywa mwaka 2012, unaonesha kuwa asilimia 92.6 ya Watanzania ambao vipimo vyao vya shinikizo la damu vina walakini, hawajaanza kutumia dawa, hali inayowafanya kuwa katika hatari ya kupata magonjwa mengine yasiyoambukiza.

Ulaji chakula bila kuzingatia kanuni za afya umeelezwa kuwa chanzo kinachochangia magonjwa hayo kuwakumba watu wengi.

Hivi sasa hospitali nyingi zinapokea wagonjwa wenye magonjwa yanayotokana na tatizo la shinikizo la damu, moyo, figo na mengine ambayo chanzo chake ni mtindo wa maisha wanayoishi.

Wataalam wa afya mara kwa mara wanashauri watu kuzingatia ulaji ulio sahihi na kufanya mazoezi ili kujikinga na maradhi hayo.

Kwa mujibu wa wataalam hao magonjwa yasiyoambukiza yanatumia gharama kubwa kuwatibu wagonjwa kulinganisha na magonjwa mengine.

Magonjwa hayo yanaweza kudhibitiwa kwa watu kufuata kanuni za afya ikiwamo pia kucheki afya zao mara kwa mara ili kujua mwenendo wao.

Kuna wakati mtu anakwenda hospitali kutibiwa tatizo lingine, lakini anapofika na kuangaliwa mwili wake anakutwa na tatizo kubwa.

Utafiti unaeleza kuwa umri wa kuishi kwa wanawake ni miaka 69 na wanaume umepungua kwa sasa wanaishi miaka 62 kwa ajili ya changamoto mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi,mazingira na mabadiliko katika maendeleo.

Magonjwa yasiyoambukiza imeelezwa kuwa ni changamoto hasa katika umri wa wazee na kila mara kumekuwa kukitolewa elimu kwa kuwashirikisha watu wenye umri huo kuwakumbusha kufanya mazoezi ya viungo ambayo yanasaidia kutoa sumu mwilini na kuimarisha mifupa na nyonga.

Moja ya mambo yanayochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo ni mabadiliko ya taratibu za kimaisha zinazohusisha matendo yanayoweza kusababisha magonjwa.

Moja wapo ni kukaa muda mrefu sehemu moja kama vile ofisini au darasani na kutojihusisha katika shughuli za michezo.

Ulaji usiofaa. Kula chakula kuzidi mahitaji ya mwili, kula chumvi na sukari kuliko mahitaji ya mwili ni vitu vinavyochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo.

Dalili za magonjwa yasiyoambukiza ni watu kujiona kuchoka bila sababu, kichwa kuuma mara kwa mara, macho kutoona vizuri, kushikwa na kizunguzungu mara kwa mara, kutokwa na damu kwenye fizi mara kwa mara, miguu na mikono kuwa na maumivu kama ya kuwaka moto na nyingi zinazofanana na hizo.

Mtu akishaona dalili hizo ni bora akimbilie hospitali na kubadili mtindo wake wa maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Jamani kikokotoo kimebainika kikohozi cha jamii, tukisikie!

**NI** kama imekuwa ndiyo kilio cha nchi. Kila ukipita neno ni hilo hilo kikokotoo. Ukizunguka huku unakutana na neno hilo. Ukiingia huku, hakuna kinachozungumzwa zaidi ya kikokotoo.

Wafanyakazi wengi wanalalamika kuhusu pesa zao walizotakiwa kupata baada ya kustaafu kazi ni kidogo mno kuliko ambayo wao wanahitaji.

Wengi wanaona kama pesa nyingi zinabaki serikalini, nao wanapata ndogo wakati ndiyo waliozifanyia kazi.

Hawakatai, lakini wanasema wao wafanyakazi wanataka asilimia nyingi ya pesa za mafao, yaani kikokotoo kiwe na asilimia kubwa upande wao kwani kipindi hicho wanazihitaji zaidi kwa sababu kwanza wanakuwa wameshastaafu kazi.

Pili, nguvu zimeanza kuwaishia na hawawezi kufanya kazi kwa nguvu ile ile ya mwanzo, hivyo walikuwa wanahitaji kuwekeza kwenye biashara zingine au kufungua kampuni, hivyo wasingeweza kufanya hivyo kwa kikokotoo kilichopo.

Wafanyakazi wengi wa sasa akili zao zipo kwenye kuwekeza zaidi, tofauti na wale wa zamani ambao walikuwa wanachukua pesa hizo kwa ajili ya kujikimu tu kimaisha kwa maisha yao waliyobaki.

Miaka ya sasa fursa zimefunguka, kuna fursa nyingi sana ambazo wanaziona kama vile kilimo, ufugaji, biashara, hivyo wanahitaji kiasi kikubwa cha pesa kwa ajili ya kuwekeza, kitu ambacho kwa kikokotoo cha sasa wanaona kama hawatendewi haki, kwani kiasi kinachobaki huko, kingeweza kuwazalishia pesa zaidi na kuwapatia faida kama wangekuwa nazo mikononi.

Hali hii ndiyo imesababisha kilio cha kikokotoo kila kona, wakitaka serikali ifanye marekebisho.

Tumeona juzi, Sikukuu ya Wafanyakazi, Mei Mosi, wamekazia mkazo zaidi kwenye kikokotoo kuliko hata nyongeza ya mishahara.

Akijibu hilo kwa wastaafu na wastaafu watarajiwa, Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango aliahidi kuwa kilio chao hicho kitafanyiwa

> **Wafanyakazi wengi wa sasa akili zao zipo kwenye kuwekeza zaidi, tofauti na wale wa zamani ambao walikuwa wanachukua pesa hizo kwa ajili ya kujikimu tu kimaisha kwa maisha yao yaliyobaki.**

uchambuzi zaidi.

Akasema serikali imepokea hoja kuhusu kubadilishwa kwa kanuni ya kikokotoo cha wastaafu kwa ajili ya kuifanyia uchambuzi zaidi kwa kuwa wafanyakazi hawaridhishwi.

Hata Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi, siku chache zilizopita akiwa katika ziara ya mikoa sita, kukagua namna serikali yake inavyowajibika kwa waliowapa kura ya kuongoza nchi, akakumbana nao wafanyakazi waliompa salamu za kikokotoo kwamba hakijakaa sawa, naye akaahidi kuzibeba kama zilivyo kufikisha mezani kwa Mama, ili zitafutiwe majibu.

Kwa hali hii inaonekana kero kubwa ya kitaifa kwa sasa ni kikokotoo kwa upande wa wenzetu waliopo kazini, maana hizo ni sehemu za pembejeo zao za maisha.

Hapa sasa ni mtihani kwa serikali na watendaji wake, kwani mtu anaposikia kelele zinavuma kutoka pembe zote za nchi, ujue kuna ujumbe ndani yake.

Unahitaji kufanyiwa utafiti wa kina na ukiufanyia utafiti, basi unataka kujua umekaaje, ili utibu kutokana na ukubwa wa jereha lilivyo, maana suala la jeraha kuwapo si mjadala tena.

Naamini kuwa sula hili litafanyiwa kazi haraka, kwani siku zote viongozi wazuri ni wale ambao wanatatua shida za watu wao, hasa zile ambazo zinawagusa watu wengi kwa wakati, moja kwa moja.

Nimalize kwa kumpa kongole la mapema, Makamu wa Rais, Dk Mpango, maana kalipokea kama lilivyo kwa wafanyakazi, ndani ya mkusanyiko wao rasmi jijini Arusha.

Hapo akaahidi kulipeleka makao makuu ya nchi watakopatikana wazito wote na majibu yatawarejea. Tusishangae, ni tabasamu la moja litawashukia wale waliokusanyika Arusha, hadi waliopiga 'stop', Nchimbi, wakimdai majibu yao.

HABARI KITAIFA

# Kampeni mlango kwa mlango TRA yavuna mabilioni

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

KAMPENI ya mlango kwa mlango inayoendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), imechangia kwa kiasi kikubwa kupaisha mapato yanayokusanywa na mamlaka hiyo.

Kwa mujibu wa TRA, Desemba, mwaka jana, iliweka historia kwa kukusanya Sh. trilioni 3.05 kwa mwezi wakati lengo lilikuwa kukusanya Sh. trilioni 2.9 kwa mwezi, sawa na ongezeko la asilimia 9.2.

Kaimu Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano wa TRA, Hudson Kamoga, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye mkutano wa 13 wa kitaaluma wa wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) unaoendelea jijini hapa.

Alisema kampeni ya mlango kwa mlango imechangia kwa kiwango kikubwa wananchi kuelewa umuhimu wa kulipa na imesababisha ongezeko la walipakodi kwa hiari na kwamba wameachana na matumizi ya nguvu.

"Moja ya sababu za kuongezeka kwa makusanyo ni mwamko mkubwa wa ulipaji kodi kwa wafanyabiashara na tumekuwa tukitumia mbinu bora na rafiki za ukusanyaji wa mapato na tulishaachana kabisa na matumizi ya nguvu kudai kodi," alisema.

Kamoga alisema ongezeko la uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini ikiwamo uzalishaji viwandani, uingizaji wa bidhaa na kuimarika kwa shughuli za utalii ni miongoni mwa vichocheo vya ukuaji wa ukusanyaji wa mapato kwa mamlaka hiyo.

Alisema filamu ya The Royal Tour ambayo Rais Samia Suluhu Hassan alishiriki kuitengeneza, imechangia kwa kiwango kikubwa kuongezeka makusanyo ya mapato kwenye sekta ya utalii hasa kwenye kodi ya ongezeko la thamani (VAT), ada za utalii na kodi ya mapato kwa kampuni zinazojihusisha na utalii.

Mkurugenzi huyo alisema uboreshaji wa uhusiano baina ya mamlaka na walipakodi, utatuzi wa migogoro ya kodi nje ya mahakama na kuongezeka kwa kiwango cha uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa njia mbalimbali nako kumechangia ongezeko la mapato.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu (2021-2023), kiwango cha wananchi na walipakodi kutii na kufuata sheria, kimeongezeka kwa upande wa matumizi ya huduma ya kuhakiki stempu ambapo kiwango cha kupakua kimeongezeka na kufikia 508,3000 kwa watumiaji wa simu za 'androids' na 'IOS'.

Kuhusu mashine za kielektroniki (EFD), Kamoga alisema mfanyabiashara yeyote anayejihusisha na kuuza bidhaa au huduma, anatakiwa kwa mujibu wa sheria kununua mashine hiyo au VFD kutoka kwa mawakala walioidhinishwa na mamlaka hiyo.

Alisema baada ya kununua mashine hiyo, mfanyabiashara anatakiwa kuitumia mashine hiyo kutoa risiti kila anapofanya biashara ili kuhakikisha anawatendea haki wateja wake kwa kuwapa risiti sahihi.

Kamoga alisema awamu ya kwanza ya matumizi ya mashine hizo, ilianza Julai, 2010 na ilihusisha wafanyabiashara waliosajiliwa na VAT na kwamba mwaka 2013 na awamu ya pili ilianza ikihusisha wafanyabiashara wasiosajiliwa kwenye VAT ambao mauzo yao ghafi ni shilingi milioni 14 kwa mwaka.

Alisema kuanzia Februari, 2022 kiwango cha mauzo ghafi cha mfanyabiashara kwa ajili ya kununua mashine za kielektroniki kilishushwa kutoka Sh. milioni 14 hadi milioni 11 kwa mwaka.



Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Shirika la Afya la Africa Academy for Public Health, Dk. Marry Sando, akizungumza wakati wa warsha ya utafiti wa afya ya akili kwa vijana, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Sarea. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Madai wastaafu EAC yatua tena bungeni

**Na Vitus Audax,** DODOMA

BUNGE limeiagiza serikali kufanya mapitio ya taarifa za wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kabla ya kuvunjika mwaka 1977 na kuja na majibu ya waliolipwa stahiki zao na wanaodai ili walipwe stahiki zao haraka iwezekanavyo.

Agizo hilo la Bunge limetolewa jana bungeni na Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson baada ya swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Hawa Mwaifunga aliyetaka kujua hatima ya malipo ya stahiki za wastaafu hao aliowataja kuzidi kuhangaika kila uchwao.

Mwaifunga alisema wastaafu hao wanahangaika kutoka mikoa mbalimbali kufuata haki yao katika Jiji la Dar es Salaam mara kwa mara, lakini wanarudi bila mafanikio.

Alihoji kuwa serikali inatoa kauli gani kuhusu malipo ya wastaafu hao ili waweze kupata stahiki zao kama zipo.

Akijibu swali hilo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alikiri kuwapo kwa Watanzania waliokuwa wafanyakazi katika jumuiya hiyo kabla ya kuvunjika mwaka 1977 ambao walikuwa wakidai stahiki zao za kiutumishi.

Alisema Ofisi yake pamoja na Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje zimekuwa zikipokea malalamiko hayo na wanayafanyia kazi kwa kuwaelekeza waende kwa waajiri wao ili kupata stahiki husika.

Alisema kumbukumbu walizonazo ni kwamba wapo waliowasilisha madai pamoja na nyaraka na wameshalipwa na kutaka kama wapo ambao hawajalipwa wawasilishe taarifa zao.

"Sasa kwa kuwa Mbunge anataka hao wanaohangaika na hawajapewa haki zao na kwakuwa serikali yetu inatenda haki kwa kila anaye stahili basi kama wapo wawasilishe madai hayo kwa mwajiri wao ili tathmini inafanywa na kama haki ipo watapewa haki zao," alisema Waziri Mkuu. Akitoa maelekezo ya Bunge Spika wa Bunge, Tulia Ackson alisema; "hili swali huwa linakuja na linarejea mara kwa mara, niutake upande wa serikali ukaangalie kwenye nyaraka kwamba wapo wanaodai?"

"Kwasababu nyaraka za waajiriwa wa kipindi hicho zipo watazamwe kama wote walishalipwa na kama wapo wanaodai walipwe kwasababu haya maswali yanaendelea kurejea na pengine wapo ambao wanadai na walishafariki na wengine wapo hai na bado wanajipa moyo kwamba kuna wanachodai kumbe hakuna," alisema Dk. Tulia.

Aidha, alisema ni bora serikali itazame na kuja na majibu kuwa hakuna anayewadai ili wabunge wanapofuatwa na hao wastaafu wawape majibu kwamba serikali imesema hakuna wanaoidai au serikali ijipe muda wa kutazama suala hilo na kutoa majibu ya moja kwa moja ili lifikie ukomo.

"Mje mseme liishe kwasababu hii jumuiya ilikufa siku nyingi na hii tulionayo sasa ni mpya na hao watu ni wazee sana si vyema kuendelea kudai haya madai," alisisitiza Dk. Tulia.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Bashungwa aagiza mkandarasi kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) Kinondoni, Mohamed Senkondo, kumshikilia Meneja Mradi wa Kampuni ya China Railway Seventh Group (CRSG), anayetekeleza ujenzi Daraja la Mpiji Chini (mita 140) pamoja na barabara unganishi (kilomita 2.3), ahojiwe na kuchukuliwa hatua kwa kuchelewa kuanza ujenzi huo.

Bashungwa alitoa agizo hilo juzi mkoani Dar es Salaam baada ya kukagua athari za mvua pamoja na eneo litakapojengwa daraja la Mpiji Chini ambalo litaunganisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kutoridhishwa na sababu za kuchelewesha maandalizi ya kuanza ujenzi.

"Hatuwezi kuendelea kubembelezana. Mkandarasi huyu amekuwa mbambaishaji katika miradi yake na huu ni mradi wa tano. OCD nakukabidhi mkandarasi huyu akatoe maelezo na awape mkataba alioutia saini ili tuanze kumchukulia hatua," alisisitiza.

Bashungwa alisema mkandarasi huyo amekuwa mbambaishaji katika utekelezaji wa miradi mingine ya barabara zikiwamo Sanzate - Nata mkoani Mara, Kibaoni - Mlele mkoani Katavi,


Amani Mahoro - Luanda mkoani Ruvuma na pamoja na miradi mingine ambayo amepewa kazi ya ujenzi.

Bashungwa alimtaka mtendaji mkuu wa kampuni hiyo kufika ofisini kwake na kueleza kuwa serikali itaendelea kumbana mkandarasi huyo kuhakikisha analeta mitambo na wafanyakazi wanaotakiwa katika mradi wa Daraja la Mpiji Chini ili kiangazi kitakapoanza, ujenzi wa daraja hilo uanze mara moja.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam, Mhandisi John Mkumbo, alisema mkataba wa ujenzi wa daraja na barabara unganishi ulitiwa saini Januari 30, 2023 na mkandarasi kukabidhiwa eneo la ujenzi Mei 22, 2023 na mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi 24 kwa gharama ya Sh. bilioni 21.

Mhandisi Mkumbo alisema vifaa vilivyoletwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ni asilimia 46 ya vile vinavyohitajika kwa mujibu wa mkataba pamoja na wataalamu sita kati ya 10 wanaotakiwa kimkataba na kwa ujumla, mkandarasi amefanya maandalizi ya ujenzi kwa asilimia 58.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, alisema daraja hilo linaunganisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kupitia vijiji vya Maputo na Kiembeni na likikamilika litakuwa mkombozi mkubwa kwa kuwa ni muda mrefu wananchi wamekuwa wakizunguka mwendo mrefu kuingia na kutoka nyumbani kwenda kazini na hata kufuata huduma za kijamii.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kushoto), akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Helium One, Lorna Blaisse (katikati) na Mkurugenzi wa Fedha na Biashara, Graham Jacobs (kulia), kabla ya kuingia bungeni jijini Dodoma juzi, kufuatilia Bajeti ya Wizara hiyo ya mwaka 2024/2025. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kundi la wafanyabiashara Saudia kutua Dar

**Na Joseph Mwendapole**

UJUMBE wa wafanyabiashara kutoka Saudi Arabia, unatarajiwa kufika nchini hivi karibuni kuangalia fursa mbalimbali za uwekezaji na ubia na wenzao wa Tanzania.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mauzo ya Nje wa Saudi Arabia, Abdulrahman Al Thukair, alipokuwa akishiriki mjadala kuhusu mageuzi ya nishati duniani.

Alikuwa akizungumza wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani unaoendelea jijini Riyadh, Saudi Arabia, ambao unahudhuriwa pia na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, na ujumbe wake.

Alisema nchi hiyo inafahamu kuhusu fursa mbalimbali zilizoko Tanzania, hivyo ataongoza ujumbe wa wafanyabiasha na wawekezaji wakubwa wa nchi hiyo kuja nchini Tanzania kwa lengo la kujionea fursa hizo.

Dk. Kijaji, aliwahimiza na kuwahamasisha wafanyabiashara wa Saudi Arabia kuongeza kasi ya kununua bidhaa kutoka Tanzania pamoja na kuja kuwekeza nchini.

Alisema Tanzania imepiga hatua kuzalisha na kusambaza umeme vijijini ambapo zaidi ya asilimia 95 vimeunganishwa na umeme. Waziri Kijaji alitoa wito kwa nchi zilizoendelea kiviwanda kuunga mkono juhudi hizo ili kuimarisha uzalishaji viwandani kwa mataifa yanayoendelea.

Dk. Kijaji anaongoza ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo unaowajumuisha Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Biashara, Sempeho Manongi, Mkurugenzi wa Bodi ya Maghala, Asangye Bangu, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Deo Shayo, Kamishna wa Fedha za Nje, Rashed Bade na maofisa waandamizi wa Ubalozi wa Tanzania- Riyadh Saudi Arabia.

# CWT Muheza kuendelea kutetea maslahi ya walimu

**Na Steven William,**
MUHEZA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema kitaendelea kutetea walimu wilayani hapa ili kupata maslahi yao kutoka kwa mwajili wao.

Pia, kimeitaka serikali kurudisha kikokotoo cha zamani cha asilimia 50 kwa kuwa watumishi wanakilalamikia kikokotoo kipya cha sasa asilimia 33.

Hali hiyo imekuja kutokana na malalamiko ya wafanyakazi kuhusu mfumo huo mpya wa kikokotoo na kudai kuongezeka mshahara kutokana na maisha kuwa magumu na kwamba chama hicho kinaendelea kuishauri serikali kurudisha kikokotoo cha zamani cha asilimia 50.

Katibu wa CWT, Wilaya ya Muheza, Seleman Mashaka, aliyasema hayo juzi katika maadhimisho ya sherehe ya wafanyakazi Mei Mosi yaliyofika kimkoa wilayani Korogwe.

"Kikokotoo kipya kimetokana na sheria mpya ya hifadhi ya jamii, ambayo inaelekeza mstaafu kulipwa mafao ya mkupuo kwa asilimia 33, huku 67 inayobaki kulipwa kama pensheni kwa miaka 12.5 ambapo watumishi wanalalamikia suala hilo," alisema Mashaka.

Alisema kuwa Rais Dk. Samia Suluhu ni msikivu watumishi wana uhakika suala hilo atalipatia ufumbuzi kurudisha mafao ya zamani kwa wastaafu ya asilimia 50.

Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Muheza, Mashauri Kanyama, alisema kilio cha watumishi wa serikali kimekuwa kikubwa kuhusu kikokotoo kipya na wengine wameshikwa na maradhi baada ya kustaafu.

Alisema watumishi wengine wamestaafu kazi kwa kutegemea kupata kiinua mgongo chao cha fedha wajenge nyumba wanaambulia kidogo hata kujenga hawawezi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Batilda Burian, alisema amepokea mabango ya maandamano katika uwanja wa TTC wilayani Korogwe kutoka kwa wafanyakazi kukataa kikokotoo kipya na kutaka cha zamani cha asilimia 50.

Aliwataka watumishi wa serikali na taasisi za umma kufanya kazi kwa bidii ili kumsaidia Rais Dk. Samia Suluhu kwa kuwa yupo pamoja na watumishi wote wa serikali kusikiliza matatizo yao.

# Watoto 2,730 mazingira magumu 'waula'

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WATOTO 2,730 wilayani Barabati Mkoa wa Manyara wameingia katika historia ya kujiajiri na kuajiriwa baada ya Shirika la Compassion International kuwakwamua kutoka mazingira magumu waliyokuwa wakiishi na familia zao.

Ni baada ya shirika hilo kuwapatia elimu kuanzia ya msingi, sekondari, ufundi na vyuo vikuu nchini.

Pamoja na mambo mengine, shirika hilo pia limejitosa kuwatetea watoto wengine wa familia hizo dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia kwa kuwalipia gharama za mawakili wa kusimamia kesi zao wilayani humo.

Hayo yalisemwa kwenye Maadhimisho ya Miaka 25 ya Shirika hilo nchini na viongozi wake wa Babati. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni Malezi bora kwa ulinzi wa Mtoto"

Awali Mwenyekiti wa Klasta ya Babati, Jonathan Mbesere akizungumza na Nipashe baada ya kupanda miti katika Shule ya Msingi Babati, alisema wanafanya kazi ya kumsaidia mtoto kutoka katika umaskini kwa kumpatia elimu na kujitegemea akiwa na maadili ya kimungu kupitia vituo vya kuwalea vya kanisa. Alisema mtoto akifanyiwa unyanyasanyaji, shirika hilo litahakikisha anapata haki yake kwa kumtafuta wakili wa kusimamia kesi hadi hukumu kwa gharama zake.

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi Mhasibu wa Compassion International kutoka Kanisa Anglican, Lilian Gwatema, alisema watoto 1,482 wamehitimu ngazi tofauti za elimu toka shirika lianzishwe mwaka 1999. Lilian, alisema shahada walihitimu 88, stashahada 106, astashahada 106, kidato cha sita 34, cha nne 358, darasa la saba 520, vyuo vya ufundi 178 na walioendelea na elimu baada ya kuhitimu 94.

Alisema walioajiriwa 580 kati ya hao Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) 28, uhazili 14, udereva 40, uuguzi 34, utawala 28, maabara 22, udaktari 20, ualimu 58 na kazi nyingine 396.

Kwa upande wa waliojiajiri 668 wamo wafanyabiashara ndogo ndogo 106, uchomeleaji vyuma 34, ufundi cherehani 38, ufundi magari na pikipiki 98, ufundi seremala 24, ufundi uwashi 40 na shughuli nyinginezo 328.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Barabara, Lazaro Twange, Makamu Mwenyeki wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Samweli John aliwaomba watoto kukataa ukatili unaofanyika.

"Yeyote atakayeona jambo la ukatili aripoti dawati la jinsia polisi au kwa ustawi wa jamii na elimu juu ya ukatili inaendelea kutolewa ngazi za jamii,"alisema.

Mkuu wa Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania ( KKKT) Jimbo la Babati, Mchungaji Roberth Mallya, alisema kuna wachungaji ambao wamelelewa na Compassion International tangu wakiwa na umri mdogo na sasa wanasimamia makanisa.

Mallya aliitaka jamii isiwafiche watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili waweze kupatiwa elimu na ujuzi.

Mmoja wa wanufaika, Catherine Thomas, alisema shirika hilo limekuwa likiwapatia usafiri wa baiskeli wanafunzi wanaotembea umbali mrefu na mahitaji mengine.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhoka (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Ofisa Mwandamizi wa masuala ya jamii na maendeleo ya kiuchumi wa kampuni ya GGML, Ruth Mharagi alipotembelea banda la GGML katika maonyesho ya afya na usalama mahali pa kazi, jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ambana DED, aamuru mhandisi akamatwe

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya (DED) ya Same mkoani Kilimanjaro, Jimson Mhagama ameagizwa kumchukulia hatua Mhandisi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mtii kwa tuhuma za uzembe na kusababisha baadhi ya majengo kujengwa chini ya kiwango.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa WIlaya hiyo, Kasilida Mgeni baada ya kukagua ujenzi wa majengo hayo na kuibaini kuwepo kwa nyufa, hivyo kutishia usalama wa maisha ya wafanyakazi na wananchi wanaopata huduma za matibabu kwenye kituo hicho.

Vilevile, Kasilida aliamuru kukamatwa kwa mkandarasi wa mradi huo kwa kushidnwa kujenga ujenzi wa majengo hayo na kubababisha dosari hizo. "Siwezi kukukabali uzembe wa aina hii, nimekuja hapa zaidi ya mara tatu simkuti, mhandisi wa halmashauri anawaacha mafundi peke yao na huyu mkandarasi aliyekuwa akijenga hapa pia akamatwe popote alipo kwa uzembe huu," alisema na kusisitiza kuwa: " Kama msimamizi mkuu wa miradi kwenye Wilaya ya Same sitakubali hujuma ya aina hii kuendelea."

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya, kwenye miradi mingine ambayo amekuwa akitembelea, amebaini kuwa mhandisi huyo anakwenda siku moja kabla ya ziara zake.

" Hii inaathiri utendaji miradi mingi kwa sababu inachelewa kukamilika kwa wakati kwa kuwa hakuna ufuatiliaji wa karibu kwa wataalam ambao wanalipwa fedha na serikali kwa kazi hiyo," alisema. Serikali imetoa zaidi ya SH. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

Akizungumza katika mkutano wake na wananchi, Kasilida aliwahimiza kujitokeza kwa wingi kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchini mwaka huu ili watumie haki yao ya kuchagua viongozi na kuchaguliwa.

# Serikali yatoa 300m/- ujenzi kivuko Sokoni 1

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo amesema Serikali imetenga Sh. milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa kivuko kinachounganisha Mtaa wa Longdong na Lolovono Kata ya Sokoni 1 jijini hapa.

Gambo aliyasema hayo juzi wakati wa ziara yake ya kata kwa kata anayoendelea kufanya katika Jimbo la Arusha Mjini kwa lengo la kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Mtaa wa Long'dong Kata ya Sokoni One, Gambo Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wamemuahidi kuanza ujenzi wa kivuko hicho siku chace zijazo.

"Nitaendelea kushirikiana na viongozi wengine wa serikali ngazi za kata na mitaa kutatua kero mbalimbali ili wananchi mpate muda wa kufanya shughuli zenu za maendeleo," alisema Gambo.

Aliahidi kujenga matuta katika Barabara ya Mnara wa Voda inayounganisha barabara ya Kata ya Sombetini na Murieti (Morombo) ili kudhibiti ajali kwa wanafunzi kugongwa na vyombo vya usafiri wakati wa kuvuka.

Diwani Saruni Olody, alisema barabara nyingi za kata yake ni mbovu na kwamba Halmashauri ya Jiji la Arusha imekuwa ikitoa greda kwa siku moja kwa ajili ya kutengeneza barabara, hivyo kushindwa kukidhi mahitaji.

"Tumekuwa tukiomba magreda halmashauri kama madiwani ili kukarabati barabara zetu, kwa bahati mbaya kila diwani alipewa greda kwa siku moja," alisema.

Alisema baada ya kukabidhiwa, lilianza kutengeneza Barabara ya Lolovono na kwamba kwa Barabara ya Kishingoni ilishindikana kwa kuwa ilikuwa jioni.

" Haikuweza kulima Barabara ya huku Longdong na kumaliza, tunaendelea kupambana kadri ya uwezo wetu Ili kuinusuru miundombinu ya barabara zetu," alisema Olody.

Mkazi wa Mtaa wa Long'dong, Norah Mollel alisema ujenzi wa kivuko hicho utawapunguzia gharama, kubana matumizi ya fedha na kuokoa muda kwa kusafiri kwa muda mfupi.

"Hiki kivuko ni muhimu mno kwa maisha yetu, ukiangalia wanafunzi wengi wa Long'dong wanavuka korongo kuelekea Lolovono ambako kuna shule nyingi, pia kuna vituo vya afya ni shida kupata huduma hizo wakati wa mvua kutokana na korongo kujaa maji," alisema.





# Wachimbaji waelimishwa madhara ya zebaki

**Na Neema Emmanuel,** MISUNGWI

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali wameanza kutoa elimu ya matumizi sahihi ya zebaki kwa migodi ya dhahabu Kanda ya Ziwa.

Akitoa elimu hiyo kwa wachimbaji wa migodi ya Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Meneja wa Usajili wa Kemikali na Maabara za Kemia Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Musa Kazumila, alisema inatokana na matakwa ya mkataba wa Minamata.

Kazumila, alisema mkataba huo unataka kutekeleza matakwa, moja likiwa la kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Alisema wameanza na wachimbaji wa migodi ya Chata, Shokeraera, Shilalo na Luhala katika Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

Alisema katika mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na kuratibiwa na NEMC, Mkemia Mkuu amepewa jukumu la kutoa elimu ya usimamizi salama na matumizi salama ya zebaki kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya mwaka 2003 kuhusu usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani, ikiwemo zebaki.

Alisema lengo la elimu hiyo pia ni kuwajengea uwezo wachimbaji na watumiaji wa zebaki wa kutambua jinsi inavyoingia mwilini, madhara yake na namna ya kujikinga.

Dereki Masako wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dodoma, alisema madhara ya zebaki yanatokea wakati wa usagaji mawe na kudondosha matope ili ikamate wakati wa kuchukua kusanyiko la kukamua kwa kitambaa na kusambaa ardhini na hewani.

Masako, alisema ni vema wachimbaji wakatumia vifaa kinga ili kujilinda dhidi ya athari za zebaki ambazo ni kuharibu mfumo wa fahamu, kushindwa kuhisi, kukakamaa kwa mwili, macho na kuharibika figo.

Alisema zebaki pia huathiri ukuaji wa mtoto kwa mjamzito kupita kondo la mama, kupoteza nguvu za kiume, msongo wa mawazo, mwili kuwasha na kupungua.

# Wazazi, walezi waachisha watoto shule

## - Wawapeleka machungani, waozesha

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAZAZI na walezi katika Kata ya Mwamala Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wanadaiwa kuwatorosha wanafunzi wavulana kwenda mikoa ya Rukwa na Tabora kuchunga mifugo na wasichana kuozwa ili kukabiliana na hali ngumu ya maisha kutokana na umaskini

Akizungumza na Nipashe, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Igegu, Leme Solo alieleza namna wanavyoshirikiana na wazazi kukabiliana na utoro kwa wanafunzi ili kuhakikisha wanamaliza masomo yao na kutimiza ndoto zao.

Solo, alisema wanafuzi wa wavulana wanaongoza kwa kuacha masomo ikilinganishwa na wasichana.

Alisema wanapofuatilia wanakuta wazazi wao wamewatorosha na kuwapeleka Rukwa na Tabora kufanya kazi ya uchungaji wa mifugo na kulipwa ujira kwa ajili ya kuendesha familia wanazotoka. Solo, alisema wanafunzi wasichana wamekuwa wakirubuniwa kufanya vibaya mitihani yao ya mwisho kwa kuandika majibu yasiyo sahihi na matusi na wale wanaofaulu wazazi wanagoma kuwapeleka sekondari kwa kigezo hawana uwezo wa kuwasomesha.

"Wanafunzi wanaofanya haya na kutoroshwa ni wale wanaotoka katika mazingira magumu, na wengi unapowafuatilia unakuta wanalelewa na mzazi mmoja au ndugu zao, hivyo anakosa mtu wa kumsukuma kuendelea na masomo na mwisho wake anakosa kujua umuhimu wa elimu na kutokomea kutafuta maisha angali mdogo," alisema.

Mwalimu wa Malezi wa Shule ya Sekondari ya Kaselya, Theodora Mdagachule, alisema kuna wazazi wamekuwa wakitumia mifano ya waliohitimu elimu za vyuo vikuu kuwa wako mitaani kwa kukosa ajira kuwashawishi watoto wao wasisome.

Mdagachule, alisema wameanzisha klabu za wanafunzi shuleni ili kukabiliana na tatizo hilo.

Hata hivyo, alisema wengi wao wameelimika na kuwasilisha malalamiko ya wazazi wao kuwalazimisha kuolewa na kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamala, Suzana Kayange alisema kuwa amekuwa akishirikiana na watendaji na wenyeviti wa vijiji kuwaelimu wazazi umuhimu wa elimu kwa watoto wao na kuachana na tabia ya kuwarubuni ili wakatishe masomo.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (katikati), akizungumza wakati wa ufungaji wa mafunzo ya maofisa tarafa na watendaji wa kata, mjini Musoma mapema wiki hii. Kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Ibrahim Minja na Mtendaji wa Kata ya Machochwe, Wilaya ya Serengeti, Bernadetha Joseph. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC akemea ukatili kwa wanawake, watoto

**Na Timothy Itembe,** MARA

MKUU wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Kanali Maulid Surumbu amekemea vitendo vya ukatili kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu kutokana na kuichafua sura ya Tarime.

Kanali Surumbu alisema hayo juzi wakati akifunga semina ya Sensa ya Watu na Makazi kwa viongozi wa Serikali, siasa, watendaji na makundi maalum mkoani hapa.

"Nakemea matukio ya ukatili wa kijinsia ambayo yanachafua taswira ya wilaya naomba mamlaka zinazohusika kuchukua hatua stahiki kwa wote ambao wanabainika kutenda matukio hayo, " alisema Surumbu.

Aliwataka viongozi hao kutoa taarifa wanapokwama kutekeleza majukumu yao huku akisisitiza ukusanyaji mapato ya halmashauri upewe kipaumbele kwa ajili ya maendeleo.

Aliwataka kushughulikia kero za wananchi kwa wakati na kusimamia ulinzi na usalama kwenye maeneo yao ili kuendelea kudumisha amani na utulivu hususani mpakani mwa Tanzania na Kenya ili wananchi waishi kwa amanii.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara aliiomba serikali kukarabati miundombinu ya barabara zilizoharibiwa na mvua ili kupunguza adha ya usafiri na usafirishaji wananchi.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya Tarime, Daud Ngicho aliwataka washiriki wa semina hiyo kuwa mabalozi kwa wengine ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mtakwimu Mwandamizi Taifa, Deogratius Malamsha, alisema Mkoa wa Mara una watu milioni 2.4, kwa mujibu wa sense hiyo ya mwaka 2022, idadi ambayo imeongezeka kutoka milioni 1.7 mwaka 2012.

Malamsha alisema kuwa Halmashauri ya Tarime, inaongoza kwa kuwa na watu 404,848 na kuwataka kutumia ongezeko hilo la watu kuongeza uzalishaji.



Ukurasa 14

Nchimbi alipotumia ziara ya kikada mikoa sita, kunadi uchumi maendeleo




**Wananchi anzeni kutathmini wabunge wenu wanachofanya**

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA MEI 3, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## SAFARI YA HAKI ZA MFANYAKAZI NCHINI

# Kutoka timtimu alizofumua Kawawa wa TFL 1955, hadi anayosawazisha Samia

• Mizizi ya SU, CSR, Baraza la Wafanyakazi, viwanda...

**Na Peter Orwa**

KATIKA kilele cha Siku ya Muungano Tanzania katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam onyesho la kumaliza tukio lilihusu gwaride la askari polisi wa kikoloni visiwani, namna walivyopata madhila.

Sinema hiyo haipishani sana na uhalisia wa yaliyowakuta watumishi Waafrika katika sehemu mbalimbali katika ajira ya kikoloni.

Inapotajwa sura hiyo, chimbuko lake ni karne ya 18, pale maendeleo hayo yalionekana sana katika nchi za barani Ulaya kama vile Ubelgiji, Uswisi na Uingereza kulikoibuka Mapinduzi ya Viwanda.

Ni hali iliyoibua bandari maarufu za Uingereza kama Derbyshire na Yorkshire, zikipokea malighafi kwa wingi kutoka nchi zilizotawaliwa, makoloni kama Tanzania yakawa vyanzo vya malighafi yanayoingizwa huko kupitia bandari hizo na nyingine maarufu.

Penye viwanda kukaibuka matabaka ya waajiriwa na waajiri, mabwanyenye wamiliki wa miradi ya viwanda. Msingi wake, wafanyakazi walionewa na kulalamika sana, hawakumiliki chochote, kasoro nguvukazi zao wakipewa maslahi na haki duni.

Ndicho kilichokuwapo upande wa wazalishaji, hasa penye makoloni kunakopatikana malighafi, pia wachache wanaotumikia serikali za kikoloni mahali hapo katika majukumu ya chini.



Rashid Kawawa; aliratibu mgomo wa wafanyakazi kitaifa, ikatikisa mno serikali ya koloni la Kiingereza wakati huo. **PICHA: MAKTABA.**

Hawakupata fursa za elimu, isipokuwa kwa wachache waliobahatika nao wengi hawakufikia ngazi za mbali.

**VUGUVUGU LA HAKI**

Ni mazingira yaliyoanzisha fukuto la kudai haki kutoka viwandani, baadhi yao jamii ya watu weusi waliohamishiwa huko ughaibuni kudai haki zao kazini.

Ndio ukawa mwanzo wa kuzaliwa harakati za kudai haki za wafanyakazi, pia baadaye vyama vya haki za watendaji siasa za vyama vya wafanyakazi zikaanza, mfano hai nchini Uingereza.

Hiyo ikavuka ng'ambo ya pili, msukumo wa wafanyakazi ukaungwa mkono na wanaharakati wa haki za wanyonge, watetezi wa watu wa chini iliyojulikana kama Fabian Society, Uingereza.

Hatima yake ilipohamia kwenye siasa, ikazaa chama cha Labour, ambacho kiitikadi hadi sasa kiko mlengo wa kushoto kwa jamii ya watu wa chini au maarufu siasa za 'wastani' wakichuana na wenye itikadi za kulia uchumi huria 'wenye nacho wamiliki.'

KOLONI TANZANIA

Nchini Tanganyika wakati huo nao kukaguswa na hali hiyo, somo la Uingereza, hasa baada ya vita kuu vya dunia na kuzaliwa Umoja wa Mataifa (UNO sasa UN). Nyendo za madai ya haki za wafanyakazi zikachukua nafasi, sambamba na uhuru wa kujitawala.

Hadi kufika mwaka 1955, kilikuwapo kilichoitwa Tanganyikia Federation of Labour (TFL), chini ya Katibu Mkuu 'jembe', Rashid Mfaume Kawawa, aliyeratibu umoja na msukumo wa kundi kubwa la watendaji kazini, ikiwamo viwanda vichache, pia mashamba ya mkonge yaliyomea kitaifa wakati huo.

Ikizingatiwa Tanganyika ilikuwa koloni la mpito (non settler colony), Wajerumani na hata baadaye Waingereza, hapakuwapo uwekezaji wa kudumu, hivyo hawakuwekeza sana miundombinu na miradi, kama ilivyo Kenya na South Rhodesia (Zimbabwe).

Kundi kubwa la Watanganyika waliajiriwa mashambani panakozalishwa malighafi na wachache ofisi ya serikali wakitumikia ngazi ya chini.

Akiwa kijana wa miaka 29 mwanaharakati na mzalendo 'kupitiliza' anayetokea masomoni Tabora, Kawawa alifanya mageuzi makubwa ya kudai haki za wafanyakazi TFL, kati ya mwaka 1955 na 1956 kukashuhudiwa mgomo mkubwa dhidi ya watawala wa Kiingereza.

Kwa namna ya pekee migomo hiyo, chini ya uratibu wa 'jembe' Kawawa kitaifa ilitikisa Shirika la Reli Afrika Mashariki (EARC) chini ya (Balozi) Christopher Kassanga Tumbo na mwingine katika Kiwanda cha Bia, Dar es Salaam,

Inaendelea Uk 12

# UCHUMI

## KUTOKA TIMTIMU ALIZOFUMUA KAWAWA WA TFL 1955, HADI ANAYOSAWAZISHA SAMIA

Inatoka Uk 11

pia vinginevyo vilizaa mafanikio.

Serikali ya kikoloni ililazimika kuridhia masukumo wa Kawawa wa TFL katika baadhi ya mahitaji ya wafanyakazi na ikaendelea kutikisa nchini hadi mwaka 1957 kulikuwapo misukumo ya migomo iliyowarejeshea wafanyakazi matunda.

Upande wa siasa, kulikuwapo nyendo zake Mwalimu Julius Nyerere na harakati za chama cha TANU kilichoanzishwa mwaka 1954 kudai uhuru, alikuwa 'amekoshwa' na nyendo za Kawawa kuwabana Wakoloni kudai haki za wenyeji.

"Aliniiita pale Lumumba (Dar es Salaam), akaniomba tushirikiane, kumbe mimi tayari siku nyingi nilishampenda (Nyerere)... tulianza kushirikiana," nakumbuka alichonisimulia Mzee Kawawa katika mazugumzo maalum naye kwake Madale, Dar es Salaam, mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Ni aina ya ubia wa pamoja, TANU na TFL zikashirikiana kuibana serikali ya ukoloni kusaka Uhuru, hata baadaye Nyerere alimshawishi Kawawa, akahamishia harakati zake ndani ya TANU mwanzoni mwaka 1957, nyendo zilizodumu hadi Uhuru wa nchi Desemba 9, mwaka 1961.

BAADA YA UHURU

Ufanisi wake Kawawa katika TFL hadi TANU katika nafasi ya Katibu Mkuu, ikamfanya aaminike sana katika tija na uzalendo na utendaji.

Kwa historia hiyo, akajikuta Nyerere baada ya uhuru anapoacha dhamana yake ya Tanganyika huru kwa muda, cheo Waziri Mkuu, akihamia TANU kukiimarisha mwaka mzima, baada ya taifa kuwa Jamhuri mwaka 1962, Nyerere akarejea serikalini katika cheo kipya Rais, Kawawa akiteuliwa Waziri Mkuu.

Tanganyika ikawa na mipango ya maendeleo ya mpito hadi kufika mwaka




Wanamuziki wa bendi ya Urafiki, waajiriwa wa Kiwanda cha Nguo Urafiki, Dar es Salaam, mwaka 1970, ambayo ilikuwa sehemu ya 'CSR' iliyotekekezwa wakati huo. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

1964, ikaundwa Jamhuri ya Muungano, upande wa Tanzania Bara ikiwa na mipango mipya ya maendeleo katika chama kimoja TANU, kikachukua majukumu ya Jumuiya ya Wafanyakazi yakihamia katika Jumuiya ya Wafanyakazi TANU (NUTA).

Ni mipango ya miaka mitano yaliyoibua mengi ya maendeleo ndani ya nchi, viwanda vingi vilijengwa hasa vya nguo, kutumia pamba ya ndani, kikiwamo Kiwanda cha Nguo Urafiki mwaka 1967.

Pia, kukafanyika Azimio la Arusha, lililotaifisha taasisi nyingi za kigeni na binafsi, zikaweka idadi kubwa ya umma kundi la wafanyakazi.

Viwanda vingi vilivyojengwa vilikuwa vya mfumo unaoitwa 'Labour Intensive' vinavyotegemea nguvukazi zaidi kutoa ajira, kuliko mashine; tofauti na zinazoitwa 'Capital Intensive' sehemu kubwa zinategemea mashine, kuzalisha, kuliko wafanyakazi.

Mageuzi hayo ya wafanyakazi, nyuma ya pazia kulikuwapo mchango wa Kawawa Waziri Mkuu, aliyedumu wa 'maneno kidogo na utekelezaji zaidi.' Mara zote akabaki ndiye mbunifu na mtekelezaji mkuu serikalini.

**SCOPO & BARAZA LA WAFANYAKAZI**

Serikali wakati inakamilisha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo mwaka 1969, ikaandaa sheria maalum ya maslahi ya wafanyakazi iliyoitwa SCOPO, ikawa maarufu sana.

Ilikuwa na vipengele vya vyeo, mishahara na hali zote za katika utumishi wa umma. Ilitafsiri kisheria Shirika ka Umma 'SU' kuwa taasisi ya serikali ina hisa kuanzia asilimia 51, ikiendana na kuundwa Tume ya Rais ya Kusimamia Mashirika ya Umma (SCOPO).

Mwaka 1971, TANU ikishika awamu ya uongozi kupitia Mkutano Mkuu Kitaifa ikapitisha agizo kuwapo mabaraza ya wafanyakazi kila mwaka katika sehemu zote za kazi nchini.

Nalo likazua shangwe makazini na limedumu hadi sasa lipo kisheria, sehemu ya sheria ya kazi nchini. Hiyo ikiwa Mpango wa Maendeleo wa Pili ukiendelea (1969-1974), serikali ikabuni kurejesha maslahi ya mifumo ya uzalishaji kwa wafanyakazi na umma kwa jumla, ambayo ndio mwanzo wa kinachoitwa sasa 'Community Social Responsibility' au CSR.

Hapo kuanzia miaka ya 1973 kukashuhudiwa utitiri wa kila taasisi kuwa na huduma za burudani, kama vile bendi za muziki na vilabu vya soka kurejeshewa umma zawadi yao, maana huduma zingine kama tiba na elimu zilitolewa na serikali bure.

Kwa wapenzi wa muziki wa dansi zilipendwa wanafahamu chanzo cha kuundwa bendi kama Urafiki 'Chakachua' na Magereza kutimiza CSR.

**CCM NA MAPYA YAKE**

Mabadiliko yaliyozaa chama CCM mwaka 1977, yaliendana na mabadiliko NUTA kuwa na OTTU, kisha kuanzia mwaka 1978, Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA) hadi ilipotimu 1992, kisha zikafuatilia TUCTA, shirikisho yenye zaidi ya vyama 10 chini yake, ndani ya mfumo huria.

Hata sheria ya 'SU' ikifanyiwa maboresho ikawa katika yale yanayohusika na majukumu ya biashara pekee kama bandari na viwanda.

**UHURIA NA WAFANYAKAZI**

Uchumi huria uliorejea kuanzia Awamu ya Pili, Rais Ali Hassan Mwinyi aliyeongeza maslahi, mathalan jumuiya ya wahadhiri.

Pia, kukawapo mfumuko wa ajira binafsi kuptia biashara na ujasiriamali na kuporomoka viwanda vya umma vilivyoshindwa kukidhi ushindani.

Iikaendelezwa katika Awamu ya Tatu, Rais Benjamin Mkapa, akiinua maslahi kama ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) wakiongezewa posho na mikopo ya magari (Mistubishi na KIA), pia pikipiki.

Muda mfupi kabla ya kuondoka madarakani, Rais Mkapa akafanya mapitio



Balozi Christopher Kassanga Tumbo; aliyefaniiosha eneo muhimu la mgomo kitaifa, shirika la reli (TRC).

ya kina akianzisha Sheria ya Ajira na Uhusiano wa Kazi ya mwaka 2004, ambayo imefanyia kazi walakini katika maisha ya kazini na kuzisimamia haki kisheria.

Zama hizo zikaendana na Awamu ya Nne kufungua ajira za umma, zikiongezwa hasa katika sekta kama za elimu na tiba.

AWAMU YA SITA

Awamu ya ya Sita sasa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anasimamia taaluma aliyoisomea Utawala wa Umma, akiimarisha stadi za ajira na sura kuu kadhaa.

Mosi, ametambua na kufanyia kazi mapungufu ya miundombinu na vifaa kazi sehemu za umma, hasa maeneo nyeti kama shule na vituo vya afya, mfano zimeshajengwa zaidi ya 300.

Ni aina ya maboresho inayoendana na mchango wa pili, kazi kubwa ya uelimishaji watumishi hao, ndani na nje ya nchi, akiwekeza mabilioni ya shilingi kibajeti kuwaelimisha madaktari hadi ngazi za shahada za uzamili.

Tatu, ni katika sura kiuchumi inayoitwa 'multiplier effect' (jambo moja kufaidisha lingine), mageuzi hayo yametanua fursa za ajira kila mwaka kote penye huduma nyeti kijamii, wakapahudumie.

Siku chache zilizopita, Rais ametangaza ajira mpya 46,000 serikalini zikifafanuliwa juzi bungeni, 12,000 ni kwa walimu hasa wa sayansi.

Pia, inaendana na kupanuliwa sekta ya kilimo, Dk. Samia alipobuni mbinu za kuinua kilimo cha kisasa kinachowafunza vijana na wanajiajiri, sasa ikipanua tafsiri ya mfanyakazi, kwenye kilimo biashara.

Dk. Samia, Rais wa kwanza mwanamke nchini, katika uzalwendo wake amepanua nafasi za jinsia yake wanaoamua serikalini, idadi yao si haba, akilenga kuinua sauti na mamlaka yao kijamii.

Mfano, siku chache zilizopita ameapisha watendaji waandamizi watatu wa kisheria kitaifa wanawake, huku mihimili mmojawapo wa dola kuamua; Spika wa Bunge ni mwanamke.

Pia, ameonyesha shauku yake kwenye kilele cha Sherehe ya Muungano, Dar es Salaam, Ijumaa iliyopita 'akikoshwa' na bendera ya gwaride siku akinena 'mara ya kwanza anaona inashikwa na mwanamama,' akiamini kufika mwaka 2030 watakuwa wengi.

Mfumo wake, Rais Dk. Samia anazunguka nje ya nchi kuvuta mitaji ya uwekezaji ikiwamo kilimo na viwanda, lengo mojawapo ni kutanua fursa za ajira, akidumisha ishara 'kinamama wanaweza kazini.'

IDADI YA WANACHAMA IKISUASUA CHINI YA ASILIMIA

## KAMPUNI YA SIMU 'YASHIKIA BANGO' BIMA MAISHA, KUINUA ELIMU UMMA KWA VITENDO

**Na Mwandishi Wetu**

INAWEZEKANA haieleweki kwa ufasaha, lakini jibu linabaki kwamba, bima ya maisha kwa jamii ni sehemu nyeti katika maendeleo ya uchumi, pia maisha ya kawaida.

Afya ya umma ni zao la mizunguko ya kawaida, katika ununuzi nyumbani, ikipaswa kulindwa na bima. Kimaisha, kutojua yajayo ni hatari kwa mtu na iko vigumu kukabiliana na hatari ya kimaisha, nje ya tahadhari mtu anadumu kuwa na hofu.

Kitaalamu, bima ya maisha, ni makubaliano kati ya mtu au kikundi cha watu na mtoa huduma za bima (kampuni) anayekubali kulipa kiasi cha pesa inapotokea kifo au ulemavu wa kudumu au wa muda mfupi, kwa mteja mlipaji pesa bima kwa kampuni ya bima, mpokeaji.

Kiwango cha malipo kinakuwapo ndani ya mkataba wa mlipaji na mpokeaji - kampuni. Bima hiyo inatajwa kuwafaa watu binafsi, kikundi cha familia, wafanyakazi au vikoba.

Hadi sasa Tanzania kunatajwa huduma hiyo inaendelea kubaki nyuma, kulinganisha na nchi nchi jirani katika sekta ya bima.

Zinatajwa takwimu za umma, kuna wanachama wa huduma hizo ni asilimia 0.53 ya watu wote sawa na Burundi; Kenya ikiongoza kwa asilimia 2.43; Rwanda (1.7%) na Uganda (0.84%).

Kwenye Bima ya Maisha, ndio kunatajwa kuwa na hali mbaya zaidi nchini, ikibeba asilimia 16 ya bima zote kitaifa nchini, kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Bima ya Afrika Mashariki ya mwaka jana.

Mkurugenzi Mkuu wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware Dk. Saqware, anaongezea kuwa mchango wa bima katika pato la taifa ni wastani asilimia mbili, akisisitiza taasisi yake ina malengo, ikipanga kuyavuka ya asilimia tatu ifikapo mwaka 2030.

**HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

Kuanzia changamoto hiyo, kampuni ya Vodacom Tanzania PLC. kupitia M-Pesa, ikishirikiana na kampuni za Sanlam Insurance na Jubilee Life Insurance, imeamua kuwekeza ubunifu wa hudum hiyo kwa watumiaji wake wa simu za mkononi, kuwapa bima ya maisha za kidijitali kwa urahisi na gharama, mradi ukiitwa VodaBima.

Ni staili ya ubunifu kutoka sekta binafsi, zikidumisha ushirikiano wa sera za umma na binafsi, uitwao PPP ulioko kisheria na kisera, kupitia bima, wasimamizi wake wadau wa teknolojia ya mawasiliano, Vodacom.

Lengo ni kutumia kiteknolojia dijitali, kupanua wigo wa huduma za bima katika maeneo mengi, hata kuongeza idadi ya watumiaji nchini.

Kitakwimu, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Nchini (TIRA) mwaka 2022, ilikuwa na kampuni 36 za bima, kati yake makubwa ni matatu yakihudumia idadi ya watu milioni 62.

Hata hivyo inatajwa, kampuni sita tu ndizo zinatajwa kutoa huduma za bima ya maisha nchini. Hapa ndipo ikaivutia Vodacom kutumia mtandao wake mpana wa simu, ikishirikiana na kampuni za bima, kupanua huduma bima kuwafikia Watanzania wengi waliko na kwa gharama nafuu.

Juma Kweba, mkazi wa Singida anathibitisha hilo akisema, "Imeufanya mchakato kuwa rahisi. Unaweza kujiunga na VodaBima kwa kutumia simu yako ya mkononi ukiwa mahali popote hapa nchini."

Anaendelea: "Ni nafuu na huokoa muda, haswa ukizingatia kuwa kampuni nyingi za bima zipo kwenye miji mikubwa."

Mkurugenzi Mkuu wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, anasisitiza: "Tanzania ni kubwa sana! Kwa hivyo, tunahimiza kampuni zaidi kujitokeza na kuingia kwenye soko la bima na kutoa huduma na bidhaa nafuu ambazo zinakidhi mahitaji ya watumiaji."

VodaBima inatoa aina mbili za bima ya maisha; ya mtu binafsi, pia kwa kikundi. Bima hiyo mpya ya maisha inaungana na zingine kama, bima ya vyombo vya moto na bima ya afya, zilizokuwapo sokoni tangu awali.

Bima ya maisha ya mtu binafsi, inatajwa kupatikana kwa ushirikiano na asasi ya Sanlam Life Insurance ikimhudumia mtu binafsi katika majanga, kama vile ulemavu wa muda mfupi, wa kudumu au mchangiaji anapofariki.

Wawekezaji hao kampuni ya simu tajwa, inafafanua gharama za bima binafsi ziko ya kuanzia Sh.100, hadi Sh. 10,000, stahiki zake zikitajwa mmiliki wa bima anaweza kulipwa mara 1,500 ya michango yake, atakapopatwa na madhara hayo yasiyotarajiwa.

Hapo kunatolewa mfano, mhusika anayechangia Sh. 1,000, anapokea fidia ya jumla Sh.1,500,000 anapofariki.

Mbia wa Vodacom, kampuni ya Jubilee Life Insurance inatoa bima ya maisha kwa kikundi kama sehemu ya huduma zake; hiyo ni pamoja na bima kwa familia, vikundi vya mikopo vya vikoba, vijana na wanawake, hivyo kunatolewa ulinzi kwa wanachama katika matukio yasiyotarajiwa kama kifo au ulemavu.

"Bima ya maisha ya kikundi ya VodaBima iliniokoa wakati nilipopoteza mzazi wangu hivi karibuni. Nilipokea fidia ya Sh. 1,500,000, ambayo ilinisaidia kutatua changamoto za kifedha zilizokuwa zinanikabili," anasema Nuru Namalla, mkazi wa Dar es Salaam.

Katika kampeni ya urasimishaji umma wa bima hizo, Mkurugenzi wa M-Pesa wa Vodacom nchini, Epimack Mbeteni, anaifafanua ni bima inayowafidia wateja; penye vifo au ulemavu, pia kwa vikundi, lengo ni kuwapa amani na ustawi wao, ikipatikana kirahisi kupitia mitandao ya pesa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Wananchi anzeni kutathmini wabunge wenu wanachofanya






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

WANGAPI mnakumbuka wakati nchi inaendeshwa na mfumo wa chama kimoja, walikuwapo wapinzani wa kisiasa, ambao hawakuwa wakiwania kuingia Ikulu?

Hivi sasa ukisikia mtu anaingia upinzani basi ujue anawania kuingia Ikulu, na si dhambi, kwa sababu chama cha siasa hatimaye malengo yake ni kuchukua dola na kuongoza nchi.

Hiyo ni halali na hakuna anayeweza kubisha hilo, pengine ndiyo sababu baada ya kuona mageuzi makubwa duniani, nasi tukaona hapana sababu ya kuendelea kuwa na mfumo wa chama kimoja.

Tulibaini, kutokuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa ni kubana watu washindwe kufunguka ya kwao waliyoona kuwa huenda yakasaidia kuongoza nchi, baada ya kubaini pengine chama kimoja kinasinzia.

Ilipoundwa Tume ya Nyalali kusaka maoni ya Watanzania waseme walikuwa wanataka nini kati ya mfumo wa chama kimoja au vyama vingi, hatimaye wengi wakasema tunataka kubaki na hicho hicho kimoja.

Waliokuwa wanaona mbali, wakaona ni bora kuwa na mfumo wa vyama vingi ili kwanza kuendana na mabadiliko duniani, pia kutoa fursa kwa watu wengine kuja na mawazo tofauti na kinzani.

Kwa hiyo, waliotaka tuendelee na chama kimoja wakawa asilimia 80, huku asilimia 20 wakipendelea kuwa na mfumo wa vyama vingi. Tafakuri ikatujibu kuwa hata kama wengi wape, lakini hata wachache wasikilizwe.

Hivyo, serikali chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi, ikasikiliza wachache na mwaka 1992, tukaachana na mfumo wa chama kimoja, kwa maana ya kuongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) peke yake.

Ndipo sasa watu wakaibuka na vyama vya upinzani, tukasikia majina kama NCCR-Mageuzi, United Democratic Party (UDP), Democratic Party (DP), Chama cha Wananchi (CUF), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Umma (CHAUMMA) na vingine vingi tu.

Uchaguzi wa mwaka 1995 tukashuhudia bungeni kuwapo kambi mbili;Tawala na Upinzani.

Watu wakachuana kwa hoja, serikali ikija na zake na wapinzani na zao, lakini lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanasonga mbele kimaendeleo.

Si kwamba kabla ya bunge hilo la vyama vingi, hakukuwapo malumbano ya hoja bungeni, la hasha! Hoja kali zilitolewa, ikiwa ni pamoja na kusikia mbunge anakamata shilingi ya wizara, pale iliposhindwa kujibu hoja au pale iliposhindwa kuridhisha.

Malumbano ya hoja, lakini kwa nia njema na maslahi mapana ya Watanzania yaliendelea. Ikafika hatua baadaye, kumekuwapo idadi ndogo ya wabunge wa upinzani ikasababisha hata kambi ya upinzani kufa na kubaki na kambi ya chama tawala chenye serikali yake na wabunge wa kuhesabu kutoka upinzani.

Mazingira hayo yakawafanya hata mawaziri wetu kupata muda mrefu sana wa shushi kiakili, kwa kutoelemewa na hoja za kuhangaisha vichwa vyao magumu kama ilivyokuwa enzi za kuwa na Kiongozi wa Upinzani bBungeni.

Kiongozi wa Upinzani Bungeni enzi hizo, kila siku za Alhamisi akibeba maswali ya kina kwa Waziri Mkuu aliyewakilisha serikali, kwa nia njema ya kulinda maslahi mapana ya Watanzania.

Leo hii siku za Alhamisi ambazo hata hivyo Waziri Mkuu anaendelea kujibu maswali, lakini imekuwa si kama zama zile.

Hivi sasa, hata mbunge akisimama, badala ya kuanza na kuuliza swali la kuibana serikali kwa niaba ya waliompigia kura jimboni wakiwamo wa upinzani, yuko anasifia kwanza kuliko waziri.

Yaani mbunge atasimama na kusifia serikali ilichokifanya jimboni mwake, zaidi ya anavyowasilisha vilio vya wananchi wake vitokanavyo na kero na kadhia za kimaisha,.

Mbunge anasahau kuwa ni jukumu la serikali kuhudumia wananchi, ambao ndio waajiri wake na kuna matatizo lukuki yanawakabili wananchi hao.

Mzazi ana jukumu la msingi kuzaa na kulea mwanawe akimhudumia kila kitu na si kusubiri atajwetajwe na mwanawe na kumzinga na sifa kedekede, kana kwamba hana wajibu wa kufanya akifanyacho cha kumlea pamoja na familia.

Tunakwenda kwenye uchaguzi, wananchi chagueni wabunge ambao watakusaidieni katika matatizo yenu na si wa kutanguliza matumbo na kutafuta uteuzi wa uwaziri na kusahau walikotoka. Ndiyo maana sasa tunataka mawaziri wasitokane na wabunge, Mnaonaje?

## UCHUMI

# KUTOKA TIMTIMU ALIZOFUMUA KAWAWA WA TFL 1955, HADI ANAYOSAWAZISHA SAMIA

Inatoka Uk 11

kuridhia masukumo wa Kawawa wa TFL katika baadhi ya mahitaji ya wafanyakazi na ikaendelea kutikisa nchini hadi mwaka 1957 kulikuwapo misukumo ya migomo iliyowarejeshea wafanyakazi matunda.

Upande wa siasa, kulikuwapo nyendo zake Mwalimu Julius Nyerere na harakati za chama cha TANU kilichoanzishwa mwaka 1954 kudai uhuru, alikuwa 'amekoshwa' na nyendo za Kawawa kuwabana Wakoloni kudai haki za wenyeji.

"Aliniiita pale Lumumba (Dar es Salaam), akaniomba tushirikiane, kumbe mimi tayari siku nyingi nilishampenda (Nyerere)... tulianza kushirikiana," nakumbuka alichonisimulia Mzee Kawawa katika mazugumzo maalum naye kwake Madale, Dar es Salaam, mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Ni aina ya ubia wa pamoja, TANU na TFL zikashirikiana kuibana serikali ya ukoloni kusaka Uhuru, hata baadaye Nyerere alimshawishi Kawawa, akahamishia harakati zake ndani ya TANU mwanzoni mwaka 1957, nyendo zilizodumu hadi Uhuru wa nchi Desemba 9, mwaka 1961.

BAADA YA UHURU

Ufanisi wake Kawawa katika TFL hadi TANU katika nafasi ya Katibu Mkuu, ikamfanya aaminike sana katika tija na uzalendo na utendaji.

Kwa historia hiyo, akajikuta Nyerere baada ya uhuru anapoacha dhamana yake ya Tanganyika huru kwa muda, cheo Waziri Mkuu, akihamia TANU kukiimarisha mwaka mzima, baada ya taifa kuwa Jamhuri mwaka 1962, Nyerere akarejea serikalini katika cheo kipya Rais, Kawawa akiteuliwa Waziri Mkuu.

Tanganyika ikawa na mipango ya maendeleo ya mpito hadi kufika mwaka 1964, ikaundwa Jamhuri ya Muungano, upande wa Tanzania Bara ikiwa na mipango mipya ya maendeleo katika chama kimoja TANU, kikachukua majukumu ya Jumuiya ya Wafanyakazi yakihamia katika Jumuiya ya Wafanyakazi TANU (NUTA).




Wanamuziki wa bendi ya Urafiki, waajiriwa wa Kiwanda cha Nguo Urafiki, Dar es Salaam, mwaka 1970, ambayo ilikuwa sehemu ya 'CSR' iliyotekekezwa wakati huo. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Ni mipango ya miaka mitano yaliyoibua mengi ya maendeleo ndani ya nchi, viwanda vingi vilijengwa hasa vya nguo, kutumia pamba ya ndani, kikiwamo Kiwanda cha Nguo Urafiki mwaka 1967.

Pia, kukafanyika Azimio la Arusha, lililotaifisha taasisi nyingi za kigeni na binafsi, zikaweka idadi kubwa ya umma kundi la wafanyakazi.

Viwanda vingi vilivyojengwa vilikuwa vya mfumo unaoitwa 'Labour Intensive' vinavyotegemea nguvukazi zaidi kutoa ajira, kuliko mashine; tofauti na zinazoitwa 'Capital Intensive' sehemu kubwa zinategemea mashine, kuzalisha, kuliko wafanyakazi.

Mageuzi hayo ya wafanyakazi, nyuma ya pazia kulikuwapo mchango wa Kawawa Waziri Mkuu, aliyedumu wa 'maneno kidogo na utekelezaji zaidi.' Mara zote akabaki ndiye mbunifu na mtekelezaji mkuu serikalini.

### SCOPO & BARAZA WAFANYAKAZI

Serikali wakati inakamilisha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo mwaka 1969, ikaandaa sheria maalum ya maslahi ya wafanyakazi iliyoitwa SCOPO, ikawa maarufu sana.

Ilikuwa na vipengele vya vyeo, mishahara na hali zote za katika utumishi wa umma. Ilitafsiri kisheria Shirika ka Umma 'SU' kuwa taasisi ya serikali ina hisa kuanzia asilimia 51, ikiendana na kuundwa Tume ya Rais ya Kusimamia Mashirika ya Umma (SCOPO).

Mwaka 1971, TANU ikishika awamu ya uongozi kupitia Mkutano Mkuu Kitaifa ikapitisha agizo kuwapo mabaraza ya wafanyakazi kila mwaka katika sehemu zote za kazi nchini.

Nalo likazua shangwe makazini na limedumu hadi sasa lipo kisheria, sehemu ya sheria ya kazi nchini. Hiyo ikiwa Mpango wa Maendeleo wa Pili ukiendelea (1969-1974), serikali ikabuni kurejesha maslahi ya mifumo ya uzalishaji kwa wafanyakazi na umma kwa jumla, ambayo ndio mwanzo wa kinachoitwa sasa 'Community Social Responsibility' au CSR.

Hapo kuanzia miaka ya 1973 kukashuhudiwa utitiri wa kila taasisi kuwa na huduma za burudani, kama vile bendi za muziki na vilabu vya soka kurejeshewa umma zawadi yao, maana huduma zingine kama tiba na elimu zilitolewa na serikali bure.

Kwa wapenzi wa muziki wa dansi zilipendwa wanafahamu chanzo cha kuundwa bendi kama Urafiki 'Chakachua' na Magereza kutimiza CSR.

### KUZALIWA CCM

Mabadiliko yaliyozaa chama CCM mwaka 1977, yaliendana na mabadiliko NUTA kuwa na OTTU, kisha kuanzia mwaka 1978, Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA) hadi ilipotimu 1992, kisha zikafuatilia TUCTA, shirikisho yenye zaidi ya vyama 10 chini yake, ndani ya mfumo huria.

Hata sheria ya 'SU' ikifanyiwa maboresho ikawa katika yale yanayohusika na majukumu ya biashara pekee kama bandari na viwanda.

### UHURIA NA WAFANYAKAZI

Uchumi huria uliorejea kuanzia Awamu ya Pili, Rais Ali Hassan Mwinyi aliyeongeza maslahi, mathalan jumuiya ya wahadhiri.

Pia, kukawapo mfumuko wa ajira binafsi kuptia biashara na ujasiriamali na kuporomoka viwanda vya umma vilivyoshindwa kukidhi ushindani.

Iikaendelezwa katika Awamu ya Tatu, Rais Benjamin Mkapa, akiinua maslahi kama ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) wakiongezewa posho na mikopo ya magari (Mistubishi na KIA), pia pikipiki.

Muda mfupi kabla ya kuondoka madarakani, Rais Mkapa akafanya mapitio ya kina akianzisha Sheria ya Ajira na Uhusiano wa Kazi ya mwaka 2004, ambayo imefanyia kazi walakini katika maisha ya kazini na kuzisimamia haki kisheria.



Balozi Christopher Kassanga Tumbo; aliyefaniiosha eneo muhimu la mgomo kitaifa, shirika la reli (TRC).

Zama hizo zikaendana na Awamu ya Nne kufungua ajira za umma, zikiongezwa hasa katika sekta kama za elimu na tiba.

AWAMU YA SITA

Awamu ya ya Sita sasa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anasimamia taaluma aliyoisomea Utawala wa Umma, akiimarisha stadi za ajira na sura kuu kadhaa.

Mosi, ametambua na kufanyia kazi mapungufu ya miundombinu na vifaa kazi sehemu za umma, hasa maeneo nyeti kama shule na vituo vya afya, mfano zimeshajengwa zaidi ya 300.

Ni aina ya maboresho inayoendana na mchango wa pili, kazi kubwa ya uelimishaji watumishi hao, ndani na nje ya nchi, akiwekeza mabilioni ya shilingi kibajeti kuwaelimisha madaktari hadi ngazi za shahada za uzamili.

Tatu, ni katika sura kiuchumi inayoitwa 'multiplier effect' (jambo moja kufaidisha lingine), mageuzi hayo yametanua fursa za ajira kila mwaka kote penye huduma nyeti kijamii, wakapahudumie.

Siku chache zilizopita, Rais ametangaza ajira mpya 46,000 serikalini zikifafanuliwa juzi bungeni, 12,000 ni kwa walimu hasa wa sayansi.

Pia, inaendana na kupanuliwa sekta ya kilimo, Dk. Samia alipobuni mbinu za kuinua kilimo cha kisasa kinachowafunza vijana na wanajiajiri, sasa ikipanua tafsiri ya mfanyakazi, kwenye kilimo biashara.

Dk. Samia, Rais wa kwanza mwanamke nchini, katika uzalwendo wake amepanua nafasi za jinsia yake wanaoamua serikalini, idadi yao si haba, akilenga kuinua sauti na mamlaka yao kijamii.

Mfano, siku chache zilizopita ameapisha watendaji waandamizi watatu wa kisheria kitaifa wanawake, huku mihimili mmojawapo wa dola kuamua; Spika wa Bunge ni mwanamke.

Pia, ameonyesha shauku yake kwenye kilele cha Sherehe ya Muungano, Dar es Salaam, Ijumaa iliyopita 'akikoshwa' na bendera ya gwaride siku akinena 'mara ya kwanza anaona inashikwa na mwanamama,' akiamini kufika mwaka 2030 watakuwa wengi.

Mfumo wake, Rais Dk. Samia anazunguka nje ya nchi kuvuta mitaji ya uwekezaji ikiwamo kilimo na viwanda, lengo mojawapo ni kutanua fursa za ajira, akidumisha ishara 'kinamama wanaweza kazini.'

Vilevile anaendelea kushikia bango usalama kazini, sasa ikifanyiwa kazi kisheria chini ya wakala rasmi ya umma OSHA.

IDADI WANACHAMA UKISUASUA CHINI YA ASILIMIA MOJA...

# KAMPUNI YA SIMU 'YASHIKIA BANGO' BIMA MAISHA, KUINUA ELIMU UMMA KWA VITENDO

**Na Mwandishi Wetu**

INAWEZEKANA haieleweki kwa ufasaha, lakini jibu linabaki kwamba, bima ya maisha kwa jamii ni sehemu nyeti katika maendeleo ya uchumi, pia maisha ya kawaida.

Afya ya umma ni zao la mizunguko ya kawaida, katika ununuzi nyumbani, ikipaswa kulindwa na bima. Kimaisha, kutojua yajayo ni hatari kwa mtu na iko vigumu kukabiliana na hatari ya kimaisha, nje ya tahadhari mtu anadumu kuwa na hofu.

Kitaalamu, bima ya maisha, ni makubaliano kati ya mtu au kikundi cha watu na mtoa huduma za bima (kampuni) anayekubali kulipa kiasi cha pesa inapotokea kifo au ulemavu wa kudumu au wa muda mfupi, kwa mteja mlipaji pesa bima kwa kampuni ya bima, mpokeaji.

Kiwango cha malipo kinakuwapo ndani ya mkataba wa mlipaji na mpokeaji - kampuni. Bima hiyo inatajwa kuwafaa watu binafsi, kikundi cha familia, wafanyakazi au vikoba.

Hadi sasa Tanzania kunatajwa huduma hiyo inaendelea kubaki nyuma, kulinganisha na nchi nchi jirani katika sekta ya bima.

Zinatajwa takwimu za umma, kuna wanachama wa huduma hizo ni asilimia 0.53 ya watu wote sawa na Burundi; Kenya ikiongoza kwa asilimia 2.43; Rwanda (1.7%) na Uganda (0.84%).

Kwenye Bima ya Maisha, ndio kunatajwa kuwa na hali mbaya zaidi nchini, ikibeba asilimia 16 ya bima zote kitaifa nchini, kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Bima ya Afrika Mashariki ya mwaka jana.

Mkurugenzi Mkuu wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware Dk. Saqware, anaongezea kuwa mchango wa bima katika pato la taifa ni wastani asilimia mbili, akisisitiza taasisi yake ina malengo, ikipanga kuyavuka ya asilimia tatu ifikapo mwaka 2030.

### HATUA ZINAZOCHUKULIWA

Kuanzia changamoto hiyo, kampuni ya Vodacom Tanzania PLC. kupitia M-Pesa, ikishirikiana na kampuni za Sanlam Insurance na Jubilee Life Insurance, imeamua kuwekeza ubunifu wa hudum hiyo kwa watumiaji wake wa simu za mkononi, kuwapa bima ya maisha za kidijitali kwa urahisi na gharama, mradi ukiitwa VodaBima.

Ni staili ya ubunifu kutoka sekta binafsi, zikidumisha ushirikiano wa sera za umma na binafsi, uitwao PPP ulioko kisheria na kisera, kupitia bima, wasimamizi wake wadau wa teknolojia ya mawasiliano, Vodacom.

Lengo ni kutumia kiteknolojia dijitali, kupanua wigo wa huduma za bima katika maeneo mengi, hata kuongeza idadi ya watumiaji nchini.

Kitakwimu, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Nchini (TIRA) mwaka 2022, ilikuwa na kampuni 36 za bima, kati yake makubwa ni matatu yakihudumia idadi ya watu milioni 62.

Hata hivyo inatajwa, kampuni sita tu ndizo zinatajwa kutoa huduma za bima ya maisha nchini. Hapa ndipo ikaivutia Vodacom kutumia mtandao wake mpana wa simu, ikishirikiana na kampuni za bima, kupanua huduma bima kuwafikia Watanzania wengi waliko na kwa gharama nafuu.

Juma Kweba, mkazi wa Singida anathibitisha hilo akisema, "Imeufanya mchakato kuwa rahisi. Unaweza kujiunga na VodaBima kwa kutumia simu yako ya mkononi ukiwa mahali popote hapa nchini."

Anaendelea: "Ni nafuu na huokoa muda, haswa ukizingatia kuwa kampuni nyingi za bima zipo kwenye miji mikubwa."

Mkurugenzi Mkuu wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, anasisitiza: "Tanzania ni kubwa sana! Kwa hivyo, tunahimiza kampuni zaidi kujitokeza na kuingia kwenye soko la bima na kutoa huduma na bidhaa nafuu ambazo zinakidhi mahitaji ya watumiaji."

VodaBima inatoa aina mbili za bima ya maisha; ya mtu binafsi, pia kwa kikundi. Bima hiyo mpya ya maisha inaungana na zingine kama, bima ya vyombo vya moto na bima ya afya, zilizokuwapo sokoni tangu awali.

Bima ya maisha ya mtu binafsi, inatajwa kupatikana kwa ushirikiano na asasi ya Sanlam Life Insurance ikimhudumia mtu binafsi katika majanga, kama vile ulemavu wa muda mfupi, wa kudumu au mchangiaji anapofariki.

Wawekezaji hao kampuni ya simu tajwa, inafafanua gharama za bima binafsi ziko ya kuanzia Sh.100, hadi Sh. 10,000, stahiki zake zikitajwa mmiliki wa bima anaweza kulipwa mara 1,500 ya michango yake, atakapopatwa na madhara hayo yasiyotarajiwa.

Hapo kunatolewa mfano, mhusika anayechangia Sh. 1,000, anapokea fidia ya jumla Sh.1,500,000 anapofariki.

Mbia wa Vodacom, kampuni ya Jubilee Life Insurance inatoa bima ya maisha kwa kikundi kama sehemu ya huduma zake; hiyo ni pamoja na bima kwa familia, vikundi vya mikopo vya vikoba, vijana na wanawake, hivyo kunatolewa ulinzi kwa wanachama katika matukio yasiyotarajiwa kama kifo au ulemavu.

"Bima ya maisha ya kikundi ya VodaBima iliniokoa wakati nilipopoteza mzazi wangu hivi karibuni. Nilipokea fidia ya Sh. 1,500,000, ambayo ilinisaidia kutatua changamoto za kifedha zilizokuwa zinanikabili," anasema Nuru Namalla, mkazi wa Dar es Salaam.

Katika kampeni ya urasimishaji umma wa bima hizo, Mkurugenzi wa M-Pesa wa Vodacom nchini, Epimack Mbeteni, anaifafanua ni bima inayowafidia wateja; penye vifo au ulemavu, pia kwa vikundi, lengo ni kuwapa amani na ustawi wao, ikipatikana kirahisi kupitia mitandao ya pesa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wananchi anzeni kutathmini wabunge wenu wanachofanya






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

WANGAPI mnakumbuka wakati nchi inaendeshwa na mfumo wa chama kimoja, walikuwapo wapinzani wa kisiasa, ambao hawakuwa wakiwania kuingia Ikulu?

Hivi sasa ukisikia mtu anaingia upinzani basi ujue anawania kuingia Ikulu, na si dhambi, kwa sababu chama cha siasa hatimaye malengo yake ni kuchukua dola na kuongoza nchi.

Hiyo ni halali na hakuna anayeweza kubisha hilo, pengine ndiyo sababu baada ya kuona mageuzi makubwa duniani, nasi tukaona hapana sababu ya kuendelea kuwa na mfumo wa chama kimoja.

Tulibaini, kutokuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa ni kubana watu washindwe kufunguka ya kwao waliyoona kuwa huenda yakasaidia kuongoza nchi, baada ya kubaini pengine chama kimoja kinasinzia.

Ilipoundwa Tume ya Nyalali kusaka maoni ya Watanzania waseme walikuwa wanataka nini kati ya mfumo wa chama kimoja au vyama vingi, hatimaye wengi wakasema tunataka kubaki na hicho hicho kimoja.

Waliokuwa wanaona mbali, wakaona ni bora kuwa na mfumo wa vyama vingi ili kwanza kuendana na mabadiliko duniani, pia kutoa fursa kwa watu wengine kuja na mawazo tofauti na kinzani.

Kwa hiyo, waliotaka tuendelee na chama kimoja wakawa asilimia 80, huku asilimia 20 wakipendelea kuwa na mfumo wa vyama vingi. Tafakuri ikatujibu kuwa hata kama wengi wape, lakini hata wachache wasikilizwe.

Hivyo, serikali chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi, ikasikiliza wachache na mwaka 1992, tukaachana na mfumo wa chama kimoja, kwa maana ya kuongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) peke yake.

Ndipo sasa watu wakaibuka na vyama vya upinzani, tukasikia majina kama NCCR-Mageuzi, United Democratic Party (UDP), Democratic Party (DP), Chama cha Wananchi (CUF), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Umma (CHAUMMA) na vingine vingi tu.

Uchaguzi wa mwaka 1995 tukashuhudia bungeni kuwapo kambi mbili;Tawala na Upinzani.

Watu wakachuana kwa hoja, serikali ikija na zake na wapinzani na zao, lakini lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanasonga mbele kimaendeleo.

Si kwamba kabla ya bunge hilo la vyama vingi, hakukuwapo malumbano ya hoja bungeni, la hasha! Hoja kali zilitolewa, ikiwa ni pamoja na kusikia mbunge anakamata shilingi ya wizara, pale iliposhindwa kujibu hoja au pale iliposhindwa kuridhisha.

Malumbano ya hoja, lakini kwa nia njema na maslahi mapana ya Watanzania yaliendelea. Ikafika hatua baadaye, kumekuwapo idadi ndogo ya wabunge wa upinzani ikasababisha hata kambi ya upinzani kufa na kubaki na kambi ya chama tawala chenye serikali yake na wabunge wa kuhesabu kutoka upinzani.

Mazingira hayo yakawafanya hata mawaziri wetu kupata muda mrefu sana wa shushi kiakili, kwa kutoelemewa na hoja za kuhangaisha vichwa vyao magumu kama ilivyokuwa enzi za kuwa na Kiongozi wa Upinzani bBungeni.

Kiongozi wa Upinzani Bungeni enzi hizo, kila siku za Alhamisi akibeba maswali ya kina kwa Waziri Mkuu aliyewakilisha serikali, kwa nia njema ya kulinda maslahi mapana ya Watanzania.

Leo hii siku za Alhamisi ambazo hata hivyo Waziri Mkuu anaendelea kujibu maswali, lakini imekuwa si kama zama zile.

Hivi sasa, hata mbunge akisimama, badala ya kuanza na kuuliza swali la kuibana serikali kwa niaba ya waliompigia kura jimboni wakiwamo wa upinzani, yuko anasifia kwanza kuliko waziri.

Yaani mbunge atasimama na kusifia serikali ilichokifanya jimboni mwake, zaidi ya anavyowasilisha vilio vya wananchi wake vitokanavyo na kero na kadhia za kimaisha,.

Mbunge anasahau kuwa ni jukumu la serikali kuhudumia wananchi, ambao ndio waajiri wake na kuna matatizo lukuki yanawakabili wananchi hao.

Mzazi ana jukumu la msingi kuzaa na kulea mwanawe akimhudumia kila kitu na si kusubiri atajwetajwe na mwanawe na kumzinga na sifa kedekede, kana kwamba hana wajibu wa kufanya akifanyacho cha kumlea pamoja na familia.

Tunakwenda kwenye uchaguzi, wananchi chagueni wabunge ambao watakusaidieni katika matatizo yenu na si wa kutanguliza matumbo na kutafuta uteuzi wa uwaziri na kusahau walikotoka. Ndiyo maana sasa tunataka mawaziri wasitokane na wabunge, Mnaonaje?

UCHUMI

# Dk. Nchimbi alipotumia ziara ya kikada mikoa sita, kunadi uchumi maendeleo

- Wateta na wakazi kupewa matatizo ya ndani
- Washangilia bajeti mabilioni ya barabara



Katibu Mkuu wa CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akisikiliza na kujibu maswali ya wananchi, waliojitokeza barabarani eneo la Mlowo, akitokea Vwawa Mbozi kwenda mkoani Songwe. **PICHA: HALFANI CHUSI.**

**Na Halfani Chusi**

DAIMA kuna uhusiano kati ya Uchumi na siasa, hata wanasiasa hupitia ndani ya jozi hizo zisizotenganishwa.

Wakati siasa inawajibika na kusimamia mwenendo wa nchi ikiwamo watu na rasilimali zao, uchumi unabaki kuwa namna umma unavyotumia rasilimali zao kidogo, kukidhi mahitaji mengi ya lazima kwa maisha ya kawaida na maendeleo.

Ndiko kunakosimama matakwa ya ziara zinazoshuhudiwa sasa za Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, (CCM) Balozi Dk Emmanuel Nchimbi na timu yake ya sekretarieti.

Hivi karibuni wakizuru mikoa sita, wakitibu matatizo yao sugu yanayowanawakabili wapiga kura wao, kuyapatia majibu kupitia serikali wanayoiongoza.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM, Amos Makalla, pia akawakumbusha wana - Mbeya lengo la ziara hiyo ni mambo manne; kuangalia uhai wa chama, ilani ya uchaguzi, maandalizi ya uchaguzi na utatuzi wa kero.

Staili yao ilikuwa kusikiliza kero kwa njia za wazi na faragha, kwa baadhi ya watu hata ikaibua furaha na bashasha.

Ni ziara iliyolengea kuangalia uhai wa chama, utekelezaji wa ilani yake ya uchaguzi, ikizingatiwa ni safari ya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwishoni mwa mwaka huu, pia uchaguzi mkuu mwakani.

Kada Dk. Nchimbi, akatumia mikutano hiyo akiahidi kufikisha hoja inayovuma sasa ya 'kikokotoo' kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hasasn, mara baada ya kupokea malalamiko hayo sehemu nyingi kutoka kwa watumishi wa umma.

Itakumbukwa, hata juzi katika kilele cha Siku ya Wafanyakazi Kitaifa mkoani Arusha, Makamu wa Rais alipokea na kuahidi serikali ilifanyia kazi.

Hivyo, Katibu Mkuu wa CCM – Nchimbi, pia ziarani akakagua maendeleo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege mkoani Rukwa, akitumia nafasi hiyo kuwataka waliopewa zabuni ya ujenzi kuongeza kasi waendane na matakwa ya makubaliano.

> **"Kama tumekubaliana ukamilike ndani ya miezi 18 kweli ufanyaji wa kazi uoneshe kasi hiyo. Hapa mmesema mlitakiwa kuwa mmetekeleza mradi kwa asilimia 15, lakini mmetekeleza kwa asilimia nane tu mmefeli asilimia saba.**

"Mkataba unasema uwanja huo unapaswa kukamilika ndani ya miezi 18, lakini mpaka sasa ni asilimia nane pekee zimekamilika hili halilingani na uhalisia wake.

"Kama tumekubaliana ukamilike ndani ya miezi 18 kweli ufanyaji wa kazi uoneshe kasi hiyo. Hapa mmesema mlitakiwa kuwa mmetekeleza mradi kwa asilimia 15, lakini mmetekeleza kwa asilimia nane tu mmefeli asilimia saba.

"Ongezeni spidi watu wa Rukwa wanataka kuona huu uwanja unakamilika ili waondokane na adha ya usafiri," anasema Dk. Nchimbi.

Pia aliahidi kuwasiliana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kutatua tatizo la uhaba wa madaktari bingwa katika eneo hilo. Ni kero iliyoibuliwa na moja ya wafuasi wa chama hicho.

Katika Mkutano huo Dk Nchimbi akachukua jukumu la kutatua kero ya kituo cha basi kimoja kuzuiliwa kutumika na kumwagiza Kaimu Mkuu wa Mkoa kutoa ruksa ya kutumia vituo vyote ambayo iliibua shangwe lililoambatana na vifijo na nderemo.

Vilevile, akawataka wafuasi wa chama hicho kuchagua viongozi wenye sifa akisistiza katika uchaguzi kuna kushinda na kushindwa.

"Wanaotusumbua katika uongozi ni wale wanaopata nafasi kisha wanajiona ni wa kina 'bwana mkubwa', ninaomba viongozi wetu kila mtu ajue yeye ni mtumishi wa umma anastahili kuwatumikia wananchi" anasema Dk. Nchimbi

Amos Makalla, naye akapokea kero 57 na kuagiza uongozi wa mkoa kuzipitia na kumrejeshea majibu ya utatuzi wake.

Makalla, anapigilia msumari hoja ya Dk. Nchimbi kuhusu uwanja wa ndege huo, kwamba wanapaswa kuwajibika 'usiku na mchana' kuhakikisha inapofika Machi mwakani uwe umekamilika.

"Bilioni 60 zimetengwa tayari mkandarasi ameshalipwa Sh. bilioni nane. Wajenge usiku na mchana nitamwelekeza na Waziri wa Ujenzi, kwa sababu tunajambo letu mwakani tunataka kushinda kwa kishindo.

Katibu wa Oganaizesheni, Issa Gavu, anawataka viongozi walioko ndani ya CCM, kujituma kwa kuwatumikia wananchi, wakijenga utamaduni wa kusikiliza kero zao.

Pia anawataka wajumbe wa mashina ya CCM, kujenga utamaduni wa kukaa vikao vya kila mwezi, akihimiza italeta chachu ngazi ya tawi kutimiza majukumu yao.

"Lazima tujenge utamaduni wa kujadiliana kwenye vikao husika ndani ya chama chetu, tusitumie vikao kama fimbo ya kuwaadhibu tusiowapenda tukienda kwa utamaduni huo tutakuwa tumeimarisha uhai wa chama chetu.

**ZIARA YA MBEYA**

Mkoani Mbeya, licha ya mvua kubwa kunyesha katika viwanja vya mkutano, umma ulikusanyika kukutana na jopo lake Dk Nchimbi, akiwataka Watanzania wote kujituma na kufanya kazi kwa bidii huku akionya kujihusisha na vitendo vya kutoa au kupokea rushwa.

Hapo, Makalla akawafafanulia kuwapo fedha shilingi bilioni 138 za kujenga barabara ya njia nne kutoka Nsalaga kwenda Ifisi, jijini Mbeya.

"Ili kuonyesha kwamba serikali inajali wananchi wake, tayari barabara imeanza kujengwa kwa ajili ya kupunguza foleni, upo mpango wa kujenga barabara kama hizo kutoka Igawa (Mbalizi), mpaka Tunduma (Songwe) na wakati wowote mkandarasi ataanza kazi" akatamka Makalla, huku akishangiliwa na hadhira.

Anasema, tangu walipoanza ziara hiyo mkoani Katavi, wamefanikiwa kusikiliza na kutatua kero za wananchi 114, kwa njia anayoiita ya kisayansi.



# Waajiri waonywa kuzuia vyama vya wafanyakazi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameonya kuwa atawachukulia hatua kali waajiri wanaozuia wafanyakazi kuanzisha na kujiunga na vyama vya wafanyakazi ili kukomesha tabia hiyo.

Dendego alitoa onyo hilo juzi wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Ikungi.

"Mimi sio muumini wa watu wanaovunja sheria, hivyo waajiri wakatakao kaidi maagizo yangu nitashughulika nao," alisema. Alisema waajiri wote mkoani humo wanatakiwa kuhakikisha wanaruhusu mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi ili kujua changamoto zinazowakabili wafanyakazi.

Alisema mabaraza hayo yatasaidia kupata ufumbuzi haraka matatizo yanayowakabili wafanyakazi na kuongeza ari na ufanisi.

"Mabaraza ya wafanyakazi yana faida kubwa kwa sababu yanarahisisha kujua changamoto za wafanyakazi zinazoweza kusababisha kuzorota kwa ufanisi wa kazi, hivyo changamoto zikitafutiwa majawabu mapema zitasaidia wafanyakazi kuongeza bidii na ufanisi kazini," alisema.

Kuhusu madeni ya wafayakazi wa Mkoa wa Singida, alisema hadi sasa zimelipwa Sh. milioni 700 kati ya Sh. bilioni 1.9 wanazodai. Dendego, alisema dhamira ya Serikali ya kulipa madeni ipo pale pale, kinachotakiwa ni uvumilivu.

Aliwataka waajiri kuacha tabia ya kuzalisha madeni mapya, ikiwemo kuhamisha watumishi bila stahiki zao.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania ( TUCTA) Mkoa wa Singida, Agnes Lucas, aliishukuru Serikali kwa kuendelea kulipa madeni ya wafanyakazi, upandishaji madaraja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ikiwamo kuwapatia vitendea kazi vya kisasa na kuongeza ari na uwajibikaji sehemu za kazi.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula (kushoto), akizungumza na wadau wa elimu, wakati wa uzinduzi wa ripoti mbili za utafiti uliofanywa na shirika la HakiElimu kuhusu kurejeshwa shuleni kwa wanafunzi waliopata ujauzito, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Uzalishaji muhogo kuongezeka nchini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la muhogo kutoka tani sita hadi kufikia 40 nchini ili kuinua maisha ya wakulima na pato.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dk. Hussein Omary alitangaza mpango huo juzi wakati akifungua kongamano la biashara na uwekezaji wa zao hilo lililofanyika jijini hapa.

Dk. Omary alitoa rai kwa wakulima kutumia mbegu bora za muhogo nchini ili kukuza tija katika zao hilo.

"Niwahamasishe wadau wa tasnia hii kuongeza uzalishaji muhogo kibiashara ili kukidhi mahitaji ya soko na kujiongezea kipato, "alisema na kusisitiza kuwa: "Kilimo cha muhogo kinalipa hivyo tunapaswa kuliwekea mikakati zao hili ili uzalishaji wake uongezeke ikiwamo kuzidi kutafuta masoko ya kimataifa." Alisema wanahitaji kuona kilimo cha muhogo kinakuwa kama ilivyo kwa mazao mengine nchini, hasa ikizingatiwa kuna uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo unaofanywa na serikali.

Hata hivyo, aliwataka wakulima wasikate tamaa pamoja na vikwazo wanavyokutana navyo kwa kuwa serikali ipo pamoja nao kukuza kilimo hicho.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Muhogo nchini (TACCASA), Mwantumu Mahiza, alisema kumekuwa na kero nyingi katika kilimo hicho na wanaamini kupitia kongamano hilo, zitatatuliwa.

Mahiza, alisema lengo lao ni kuona kilimo hicho kinapiga hatua na wakulima wanaongeza mashamba.

Alisema wakulima wamejipanga kuhakikisha wanaendeleza kilimo hicho kwa kuwa kina manufaa makubwa kwao kiuchumi.

Aliahidi kuzingatia maelekezo ya serikali ili kukuza kilimo hicho na kuwa chenye tija kwa wakulima.

# Wakufunzi famasi watakiwa kuwa wabunifu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Mganga Mkuu wa Serikali, Ziada Sellah, amewataka wakufunzi wa vyuo vya famasi nchini kuongeza ubunifu kwenye ufundishaji ili kuzalisha wataalamu wa kutosha na kupunguza malalamiko ya wananchi dhidi ya huduma mbovu.

Sellah alitoa wito huo juzi jijini hapa wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka pamoja na Maadhimisho ya Mafanikio ya Mradi wa Kuboresha Mafunzo na Huduma za Famasi nchini (MAP-QPS) awamu ya pili ulioambatana na uzinduzi wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Masiliano (TEHAMA) na ugawaji wa vitabu vya famasi.

Katika Mkutano huo ulioandaliwa na wadau wa famasia na Tume ya Kikrito ya Huduma za Jamii (CSSC), alisema famasi ni moja kati ya kada muhimu kwenye sekta ya afya, hivyo wakufunzi hawana budi kuhakikisha wanaongeza jitihada kwenye ufundishaji ili kupata wataalamu wa kuhudumia jamii.

Alisema kama wakufunzi watashindwa kusimamia wale wanaowafundisha, utoaji wa huduma za famasi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali utakuwa wa mashaka.

"Ukitoa mtaalamu mbovu tutakaye kunyooshea kidole ni wewe mkufunzi kada hii ya famasi ndiyo kada muhimu sana kwani inahusika na utoaji wa dawa na kama mtu atakosea kutoa dawa kwa mgonjwa anaweza kuharibu kila kitu hata kusababisha kifo kwa mgonjwa"alisema

Alisema hadi sasa serikali imesajili vyuo vya famasi 106. "Niwatake wafamasia muendele kujiendeleza kimasomo kwani teknolojia na vitu vinabadilika kila siku ili muendane na mabadiliko hayo mnapaswa kusoma," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji CSSC, Peter Maduki, alisema lengo la mradi huo ni kupanua na kuboresha huduma za afya na kutoa uelewa kwa jamii kuhusu sheria na sera za nchi.

Maduki, alisema mradi huo upo katika taasisi 965, za afya nchini ambazo ni vituo vya afya, zahanati, hospitali za mikoa na kikanda kama Bugando (Mwanza) na KCMC (Kilimanjaro).

Naibu Msajili wa Baraza la Famasi Tanzania, Godfrey Ngonela, alisema wanashukuru mradi huo umesadia kuboresha mbinu za ufundishaji katika vyuo vya famasi nchini.



# Watumishi wa umma 400 'kikaangoni'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya watumishi wa umma 400 nchini wamefikishwa Tume ya Utumishi wa Umma kwa tuhuma za ukosefu wa nidhamu na kutowajibika kazini kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu, Hamisa Kalombola alitoa takwimu hizo kwenye kikao kazi baina ya tume na watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kilichofanyika jijini hapa.

Jaji Kalombola alisema kuwa wameanza kuzungukia kanda zote na kuonana na viongozi na watumishi ili kutoa elimu ya namna bora ya utendaji kazi ili kuepuka migogoro inayowapeleka kwenye tume hiyo.

Alisema matatizo yanayosababisha watumishi hao kufikishwa kwenye tume hiyo yapo yanayotokana na viongozi na mengine uzembe wa watumishi wenyewe.

"Kwahiyo naomba pande zote tujitathimini kwenye hili," alisema.

Aliwataka watumishi na viongozi kuepuka migogoro ambayo inaweza ikasababisha kushuka kwa utendaji kazi na kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Mathew Kilama amewataka watumishi kila mmoja kufuata sheria za utumishi wa umma na kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya kazi ili kuepuka makosa ambayo yanaweza yakamsababishia kupelekwa kwenye tume hiyo.

Aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanatimiza wajibu wao na kudai haki ili kuepuka migogoro hiyo na kukwamisha utendaji kazi.

Aliwataka viongozi kutekeleza mahitaji ya watumishi ili kupunguza manung'uniko kwa kuwa yanapunguza morali ya kazi na kutofikia malengo.

Baadhi ya watumishi wa umma wa mikoa ya kanda hiyo, waliiomba tume hiyo kutoa elimu kwa viongozi ili kupunguza maamuzi ambayo yamekuwa yakisababisha migogoro baina yao.

Wilson Lulandala ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wanging'ombe mkoani Njombe, alisema mikutano hiyo inasaidia kuwaweka pamoja viongozi na watumishi na kujifunza mbinu sahihi za kutatua migogoro.



Polisi Kata ya Ilemi, jijini Mbeya, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Elibariki Mambuye akiwakabidhi msaada wa sare za shule na madaftari wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu wa Shule ya Msingi Lyoto, mwishoni mwa wiki. Vifaa hivyo, alikusanya kutoka kwa wadau mbalimbali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kanisa lapata mwarobaini uchafuzi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Morogoro limetoa zaidi ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya kuanzisha mradi unaojulikana kwa jina la Taka kwa Thamani ili kukabiliana uchafu wa mazingira katika kata za Manispaa ya Morogoro.

Mradi huo wa miaka miwili utaendeshwa kupitia Shirika lake la Huduma Kamilifu ya Jamii (DDSCDO) kwa kushirikiana na Manispaa hiyo na kutoa ajira kwa wanawake, vijana na makundi maalumu kupitia vikundi kazi.

Akizungumza wakati wa kutambulisha mradi huo kwa wadau, Askofu wa Kanisa hilo, Godfrey Seheba, alisema fedha hizo zimetolewa kupitia ufadhili wa Norwegian Church Aid (NCA) Tanzania.

Askofu Seheba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya DDSCDO, alisema mradi huo una lengo la kuchangia ufanikishaji wa sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na vipaumbele vitatu ukusanyaji wa mapato, taka, kuweka manispaa safi na usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Meneja Programu wa DDSCDO, Pius Ngirwa, alisema kuanzishwa kwa mradi huo kunafuatia utafiti kubaini uzalishwaji wa taka ngumu kwa Manispaa ya Morogoro kwa siku ni tani 377, kati ya hizo, asilimia 30 zinakusanywa na kuchakatwa, nyingine kugeuka kero na kusababisha uchafuzi wa mazingira.

" Kwahiyo mradi huu unaenda kupunguza taka katika Manispaa ya Morogoro kwa kuwa matokeo ya taka ngumu yamekuwa yakisababisha kuharibika kwa baadhi ya miundombinu inayopelekea mtawanyiko wa maji na kuleta mafuriko, kueneza magonjwa na kuhatarisha maisha ya viumbe hai, " alisema Ngirwa.

Ofisa Miradi wa NCA Tanzania, Oscar Halazya, alisema taka hizo zitaongezewa thamani zitakapochakatwa na kutengeneza ajira kwa vijana kwa kuzalisha chupa za maji na mafagio.

# Watakiwa kubuni mbinu kudhibiti maambukizi VVU

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya imewataka wadau wa afya kufanya utafiti wa hali ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) mkoani hapa kubaini ufanisi wa mbinu zinazotumika kudhibiti maambukizi mapya na kubuni mbinu nyingine za kudhibiti.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye kikao kazi cha wadau kilicholenga kufanya tathimini ya ripoti ya utafiti uliofanyika mwaka 2022 kuonyesha bado kuna watu wanaishi na maambukizi bila kujitambua.

Homera, alisema taarifa ya utafiti huo inaonyesha kuwa kiwango cha maambukizi katika mkoa huo ni asilimia 9.6 na unashika nafasi ya tatu kitaifa baada ya Njombe na Iringa ambayo ni ya kwanza na ya pili.

Alisema 95 tatu za udhibiti wa maambukizi hayo, zinaonyesha kuwa ya kwanza ambayo inalenga kuhakikisha asilimia 95 ya watu wanaoishi na maambukizi hayo wajue hali ya maambukizi mafanikio yake ni madogo.

Alisema utafiti huo wa 2022/2023 unaonyesha asilimia 91 pekee ya watu wanaoishi na maambukizi hayo wanazijua hali zao na kwamba takwimu hizo zinatia wasiwasi kuwa juhudi za wadau bado hazijazaa matunda.

Homera, aliwataka wadau kufanya utafiti ili kupata takwimu zenye uhalisia kwa maelezo kuwa wananchi wengi kwa sasa wanajitambua na wanajilinda hali ambayo ilitakiwa kiwango cha maambukizi kishuke.

"Lazima tutumie mbinu tulizozitumia kwenye masuala ya udumavu na ukondefu kupunguza takwimu hizi, kwahiyo nawaomba TACAIDS na wadau wengine mfanye utafiti upya maana kila mwaka tunaonekana tumefikia asilimia 91, ina maana hizi kazi zote za wadau zinaonekana hazisaidii," alisema Homera.

Aliwataka wadau kushirikiana na halmashauri kufanya tathimini za ndani ili kubaini hali ilivyo na kuongeza mbinu zaidi za kudhibiti maambukizi.

Mratibu wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Petro, aliahidi kushirikiana na viongozi wa Mkoa wa Mbeya kufanya utafiti ili kupata takwimu zenye uhalisia.

Petro, alisema watashirikisha na taasisi iliyofanya utafiti wa mwaka 2022/2023 ili kupata viashiria vingine vya maambukizi ambavyo ilibaini ili na wao wavitumie kufuatilia.

Alisema viashiria watakavyohitaji ni vile vinavyoonyesha hali ilivyo kwenye halmashauri ambako ndiko takwimu hizo ziliianzia kukusanywa.

"Ikiwezekana tutamwandikia barua Mtakwimu Mkuu wa Serikali atusaidie kuchakata takwimu zote tunazozihitaji ili tujue ukubwa wa tatizo na namna ya kukabiliana nalo," alisema Petro.

Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo inakabiliwa na takwimu za juu za maambukizi ya VVU kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu kutokana na kupitiwa na barabara kuu ya kwenda nchi za Zambia na Malawi.

## Wahofia kupokwa maeneo sokoni Mwanakwerekwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA wa Soko Kuu la Mwanakwerekwe visiwani hapa wamesema hawana uhakika wa kurejea baada ya kuondolewa ili kupisha ujenzi wa soko hilo.

Waliyasema hayo jana katika mkutano na viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa soko hilo katika eneo la Mwanakwerekwe.

Walisema wafabiashara wengi walipohama katika soko hilo na kuhamia Mwanajwerekwe C wamefilisika kwa sababu maeneo hayo hayakuwa rafiki kulinda mitaji yao.

Khalfan Said Bakari, miongoni mwa wafanyabiashara hao, alisema wakati wakijiandaa kurudi katika soko hilo jipya mitaji yao imekufa na kuiomba serikali kuwakopesha fedha kwa ajili ya kuendeleza biashara.

"Wakati huu soko hilo liko mwishoni kukamilika, lakini wafanyabishara hatuna uhakika wa kurudi katika soko hilo kuu kwa vile wamejitokeza baadhi ya watu wanasema anayetaka nafasi katika soko hilo atoe shilingi milioni moja kwa jili ya kupatiwa eneo," alisema Bakari .

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Said Hamad Ali, alisema malengo ya jumuiya ni kuhakikisha wafanyabiashara wanapata mafanikio katika biashara zao.

Ali alisema licha ya wafanyabiashara hao kuwa na changamoto ya kibiashara hasa kushuka kwa mitaji yao, wanatakiwa kuwa kitu kimoja.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Magharib B Unguja, Khamis Hassan Haji, alisema uamuzi wa serikali ni kuwarejesha kwanza wafanyabiashara waliyokuwa wakifanya biashara zao katika soko hilo na si vinginevyo.

# Vyandarua 782,000 kusambazwa sheria 314 Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

VYANDARUA zaidi ya 782,000 vinatarajiwa kusambazwa katika shehia 314 visiwani hapa ili kupambana na ugonjwa wa malaria.

Hatua hiyo imekuja baada ya Serikali ya Marekani kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kuzindua kampeni ya kusambaza vyandarua kwa ajili ya kupambana na ugonjwa visiwani hapa.

Kampeni hiyo imezinduliwa huku Waziri wa Afya Zanzibar, Dk. Nassor Ahmed Mazrui akiisisitiza jamii visiwani hapa kuchukua hatua za haraka kudhibiti ongezeko la malaria.

Akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani visiwani hapa, Dk. Mazrui alisema kuwa: "Tuna jukumu la kuhakikisha tunatokomeza maradhi ya malaria kwa lengo la kuiweka jamii yetu salama."

Alisema ripoti ya malaria inaonyesha kuwa hali ya ugonjwa huo Zanzibar ipo chini ya moja na kwamba hilo ni jambo jema na muhimu sana.

Kampeni hiyo ya kusambaza vyandarua visiwani hapa inajulikana kama "Usingizi Bul Bul" yaani usingizi wa amani, inawakilisha mkakati mpana wa kutokomeza malaria.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Craig Hart alisema kuwa: "Serikali ya Marekani ina heshima kubwa kuungana na Serikali ya Zanzibar kuanzisha kampeni ya usambazaji wa vyandarua vilivyotiwa dawa Zanzibar na kuhakikisha vinatumika ipasavyo."

Mpango huo wa usambazaji vyandarua hivyo vilivyotiwa dawa ni mwendelezo wa mapambano dhidi ya malaria visiwani hapa.

Mfumo huo usambazaji vyandarua pia utatumika kusambaza Ujumbe Mfupi wa Maneno (SMS) kwa kaya zinazopokea vyandarua, kutoa elimu juu ya matumizi sahihi na jinsi ya kuvitunza.




Baadhi ya Watumishi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) Zanzibar, wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT wawekana sawa uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT Wazalendo Taifa, Othman Masoud Othman amewataka viongozi na wanachama kushikamana ili kuhakikisha chama hicho kinapata ushindi katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

Alitoa rai hiyo wakati akizungumza na viongozi wa chama hicho kisiwani Pemba kwa ajili ya kutoa shukrani baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo.

Aliwataka viongozi hao kukubali kukosoelewa na kujikosoa na kutekeleza maelekezo ya chama na viongozi bila kujali umri.

Pia aliwataka viongozi hao kutoogopa kukosolewa na wanachama wakati wanapotekeleza majukumu yao.

Vilevile, aliwakumbusha kuwatetea wananchi na kuwaletea maendeleo kiuchumi na kijamii ili wasivunjike moyo wa kuendelea kukiunga mkono chama hicho.

Aliwataka wananchi kutokata tamaa na kuendelea na harakati za siasa ndani ya chama hicho badala ya kuvunjika moyo.

Akizungumzia kuhusu uchumi wa wananchi, Othman alisema Zanzibar inaweza kupiga hatua kubwa kwa kutumia rasilimali za ndani iwapo zitasimamiwa kwa umakini na viongozi waadilifu.

Akizungumzia zao la karafuu, alisema kwa sasa katika Kisiwa cha Pemba linavunwa si zaidi ya tani nane kwa mwaka, iwapo litaimarishwa na kusimamiwa vyema, upo uwezekano wa kuzalisha zaidi ya tani 15,000 na kuwaingia wakulima Sh. bilioni 4 kila msimu.

Akizungumzia hali ya siasa, Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema yapo matarajio ya kupata mabadiliko katika uchaguzi ikiwemo kura ya mapema, marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi na Sekeretarieti ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Zanzibar, Ismaili Jussa Ladhu, alisema hakukurupuka kuomba wadhifa huo kwani ni dhamira yake ya kweli kumsaidia mwenyekiti wa Taifa kujenga na kuimarisha chama hicho ili kupata ushindi kwenye uchaguzi ujao.

# Wanyamapori 16 wagongwa na kufariki Makuyuni

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa,** ARUSHA

WANYAMA 16 katika eneo la wanyamapori la Makuyuni lililopo Wilaya ya Monduli mkoani Arusha wamegongwa na kufariki katika kipindi cha Julai 2022 hadi sasa.

Ofisa Uhifadhi wa eneo hilo, Ruahmangi Kishe alitoa takwimu hizo wakati akizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JETI).

Alisema changamoto inayowakabili ni wanyama kugongwa na magari kunakotoka na mwendokasi wa madereva wakati wanyama wakikatisha Barabara ya Arusha kwenda Babati na kutoka Arusha kwenda Karatu.

Alisema kati ya idadi hiyo ya wanyama pori waliogongwa wawili ni pundamilia ambapo faini yake kwa mmoja ni Dola za Marekani 1,200 (Sh. milioni tatu).

Alisema waliogonga walilipa fedha hizo na faini za wanyama wengine akiwemo tembo ni Dola za Marekani 15,000, twiga Dola za Marekani 15,000, nyati Dola za Marekani 1900, pofu Dola za Marekani 1,700, tandala mdogo Dola za Marekani 2,600, fisi Dola za Marekani 550, choroa Dola za Marekani 2,800, swala pala Dola za Marekani 390 na tandala Dola za Marekani 2,200.

Alisema eneo hilo linavivutio mbalimbali na mandhari nzuri yenye kupendeza ikiwemo milima yenye mwinuko ambapo watalii wengi wanafurahia kutembelea milima zaidi ya kitu chochote.

"Pia wanyamapori tulionao katika eneo hili ni kivutio kikubwa, mnyama wa kipekee ambae analitangaza eneo hili ni choroa (jamii ya swala) ikilinganishwa na hifadhi zingine lakini pia kuna aina mbalimbali ya ndege akiwemo mbuni,"alisema Meneja huyo.

Alisema pia kuna utalii wa kiutamaduni ambapo eneo hilo limezungukwa na jamii ya kimasai na ni kivutio kwenye utalii kutokana na mila na desturi zao.

Ofisa Uhifadhi Daraja la Kwanza kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kanda ya Kaskazini, Yuthnes Godffray Nestory alisema eneo hilo ni jipya lakini linaupekee na uzuri na limejizolea umaarufu kwa watalii wengi.

Alisema eneo hilo kipindi cha nyuma lilikuwa ni muunganiko wa mashamba matatu ikiwemo amani, loldebes na lente ambapo yakitumika kwa shughuli za kilimo lakini likasimamishwa kwa shughli hizo na kwa sasa wanyama wamepata usalama wa chakula, makazi na maji kwa kutokuwa na shughuli za ujangili.

Alisema ulinzi unaoimarishwa na TAWA kusimamia eneo hilo imesaidia kupunguza migongano ya wanyamapori na binadamu na uwepo wa makundi makubwa ya wanyama wakiwemo tembo, twiga, pofu, pundamilia, simba na wanyama wengine.

Akizungumzia idadi ya watalii, Ofisa Utalii wa Makuyuni, Chacha Masase alisema kutoka Oktoba mwaka 2023 hadi sasa watalii 239 wameshatembelea eneo hilo, kati yao watalii wa ndani 187 na wa nje ni 52.

Alisema kipato kilichopatikana kutokana na wageni hao ni Shilingi milioni 11.6.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HARUNI HASSAN OMARY** anatangaza kupotelewa kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 454519 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 03/02/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBP/RB/832/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.15/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU FABIAN FAUSTINE wa MNADANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA NELSON WILSON**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 05 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 30 Mwezi 04 Mwaka 2024.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha MABOGINI Mkoa KILIMANJARO.**
**Shauri la Madai /Ndoa 2, 2021.**
**Jina la Mdai GAUDENCE VENANCE MARISHANI.**
**Jina la Mdaiwa SAUMU RAMADHANI ALLY.**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa DALALI MPONZI-GREGORY MPONZI MKAZI WA MOSHI-0628083179**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake/ yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )
Mdai **TAFADHALI FIKA MAHAKAMANI KWENYE SHAURI LA UTEKELEZAJI WA SHAURI LA TALAKA NO.2/2021.**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 mwezi 05 mwaka 2024 saa 4:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 04 Mwaka 2024

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha MABOGINI Mkoa KILIMANJARO.**
**Shauri la Madai /Ndoa 2, 2021.**
**Jina la Mdai GAUDENCE VENANCE MARISHANI.**
**Jina la Mdaiwa SAUMU RAMADHANI ALLY.**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa GAUDENCE VENANCE MARISHANI-0744208838 MKAZI WA SHABAHA –MOSHI NA MPANDA .**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake/ yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )
Mdai **TAFADHALI FIKA MAHAKAMANI UTEKELEZAJI SHAURI LA TALAKA NO.2/2021 .**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 mwezi 05 mwaka 2024 saa 4:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 04 Mwaka 2024

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**YUSUPH MASHIMBA MAGANDULA** naomba kutangaza kupotelewa na hati ya kusafiria Namba TAE489589 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mwaka 04/07/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/111828/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. ...../2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU GABRIEL HOT MWANKOTA WA...............**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA GWAMAKA GABRIEL MWANKOTA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 08 mwezi 05 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
**Imetokewa leo tarehe 19 mwezi 04 mwaka 2024.**

HAKIMU

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NA 6433 YA MWAKA 2023.**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**NAGHENJWA BOAZ MFINANGA**
**NA**
**NANCY BOAZ MFINANGA..................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 24 Mwezi May, 2024. Saa 3:00 Asubuhi. Siku ambayo Shauri hili limepangwa kusikilizwa Mbele ya Mhe. Jaji S.S.Sarwatt.
Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 30 Mwezi wa Aprili, 2024.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUZANA CONSTANTINE SHILOGILE**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 774 DXL, Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**PHQ/MOR/MOR/11166/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KELVINI SAMWELI ORIO**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T475DPL aina ya Toyota RACTIS, Chassis No. SCP1000018717, Engine No. 2SZ1581278. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/14652/2024.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL P. NSHUNJU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3097/0008 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DYNAMIC HIGH SCHOOL mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/77152/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA 14. 04 YA MWAKA 2024**
**BAINA YA CLEN MADIMILO.........MDAI**
**DHIDI YA**
**LAWRENCE URIO.........MDAIWA 1**
**JOSEPH MHANDO.........MDAIWA 2**

**KWA**
**LAWRENCE URIO**
**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa Kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 15.05.2024 saa 3:00 asubuhi kwa ajili ya maoni ya wazee wa baraza na baadae hukumu.
**ANGALIZO: -** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kuendelea kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 16 ya Mwezi Aprili, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi**
**Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Makubaliano usitishaji vita ya Gaza yakaribia

**TEL AVIV, Israel**

MAREKANI imeishinikiza serikali ya Israel na kundi la hamas kufikia makubaliano ya amani na kueleza wakati ni sasa wa kufikia hatua hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alieleza kwamba Israel na Hamas hawana sababu ya kuendelea na vita, hivyo kuna ulazima wa kusitishwa na kuwaachia huru mateka wanaoshikiliwa.

Blinken alisema makubaliano yapo mezani na Hamas wanapaswa kukubaliana nayo.

Jopo la wapatanishi wanasubiri jibu kutoka kwa Hamas kama watakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa.

Iliripotiwa kuwa makubaliano hayo yanahusisha usitishaji vita wa siku 40 na kuachiliwa zaidi ya mateka 30 wa Israel kwa kubadilishana na wafungwa wengi zaidi wa Kipalestina.

„Tumedhamiria kupata usitishaji mapigano ambao unawaleta mateka nyumbani na sababu pekee ambayo hilo halingeafikiwa ni Hamas," alisema Blinken wakati alipokutana na Rais wa Israel, Isaac Herzog, mjini Tel Aviv.

„Kuna pendekezo kwenye meza, na kama tulivyosema, hakuna ucheleweshaji, hakuna visingizio. Wakati ni sasa." Aliongeza waziri huyo.

Ofisa mkuu wa Hamas amekanusha kwamba kundi hilo ndilo linalochelewesha kuafikia makubaliano hayo mapya.

Familia za mateka zilikuwa zikiandamana nje ya Ikulu wakati Blinken akitoka ndani na kuwaambia kuwa suala la kuwaachilia wapendwa wao ndio msingi wa kila kitu wanachojaribu kufanya.

Mateka 130 kutoka miongoni mwa 253 waliotekwa nyara na Hamas wakati wa shambulio la Oktoba 7, mwaka juzi bado wanashikiliwa na kundi hilo.

Watu 34 kati yao wanakisiwa kuwa wamekufa au wameokolewa.

Wakati huo huo, shambulizi la Israel dhidi ya misafara miwili ya kutoa misaada iliyokuwa ikielekea Ukanda wa Gaza, limesababisha hasira huko nchini Jordan.

Misafara hiyo ya mashirika ya kutoa misaada ilikuwa ikielekea katika kituo cha mpakani cha Kerem Shalom na Beit Hanoun-Erez.

Msaada huo ni wa kwanza kutoka nchini Jordan kuingia kupitia kivuko cha Beit Hanoun.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Jordan, Sufyan Al-Qudah, aliiambia BBC Kiarabu kwamba upande wa Israel ulipaswa kutoa ulinzi kwa malori ya misaada dhidi ya mashambulizi yoyote.

Wizara ya Mambo ya Nje na Masuala ya Raia wa Kigeni ya Jordan, katika taarifa yake iliishutumu serikali ya Israel kwa kushindwa kulinda misafara miwili ya kutoa misaada na kuruhusu kushambuliwa ikiwa ni ukiukaji wa sheria.

*BBC*




Raia wa Israel wakiandamana kuishinikiza serikali ya Benjamin Netanyahu kuwarejesha salama mateka waliosalia mikononi mwa kundi la Hamas jana. **PICHA: REUTERS**

# Mafuriko yaua 179 Kenya, watalii wakwama hifadhini

**NAIROBI, Kenya**

WATALII zaidi ya 100 wamekwama katika hifadhi ya Maasai Mara baada ya maji ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa kuendelea kunyesha nchini Kenya.

Mvua za El Nino zinaendelea kunyesha nchini humo na kusababisha uharibifu wa barabara, madaraja na miundombinu mingine.

Jumla ya watu 179 wameripotiwa kupoteza maisha katika matukio yanayohusiana na mafuriko tangu mwezi Machi, kulingana na takwimu rasmi za serikali.

„Kuna watalii zaidi ya mia moja waliokwama katika zaidi ya nyumba kumi na mbili za kulala wageni na kambi maalum," alisema Stephen Nakola, msimamizi wa kitongoji cha Narok Magharibi

Aliongeza kwamba hizo ni takwimu za awali kwa sababu kambi nyingi hazijafikiwa.

Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya lilisema limewaokoa watu 61 waliokuwa wamekwama kwenye kambi za kitalii na nusu yao kwa njia ya anga.

„Katika kambi zingine, mahema yalichukuliwa" wakati daraja liliharibiwa," alisema kupitia mtandao wa X.

Hifadhi ya Maasai Mara ina utajiri wa wanyamapori wakiwemo simba, tembo, faru, chui, twiga, viboko na duma ambao huvutia watalii.

Usiku wa kuamkia Jumatatu, bwawa la asili katikati mwa nchi hiyo lilipasuka kutokana na kuzidiwa na maji na kusababisha maporomoko ya ardhi yaliyosomba vijiji kadhaa. Katika tukio hilo watu 50 walifariki na kuelezwa ndilo baya zaidi tangu kuanza kwa msimu wa mvua.

*RFI*

## Marekani kufanya mazungumzo kurudisha jeshi

**ACCRA, Ghana**

JESHI la Marekani linapanga kufanya mazungumzo na serikali ya Chad kwa kipindi cha mwezi mmoja yenye lengo la kufanya maboresho ya makubaliano ambayo yatatoa nafasi ya askari wake kuweka kambi nchini humo.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Jeshi la Majini la Marekani kwa Afrika, Jenerali Michael Langley, katika mkutano wa pili wa vikosi vya majini vya Afrika, au AMFS uliofanyika mjini Accra,nchini Ghana.

Alisema kuondolewa kwa wanajeshi wa Marekani nchini Chad kulitarajiwa kuwa ni kwa muda mfupi, na serikali ya nchi zote mbili ziliwasiliana kuendeleza ushirikiano wa kiusalama baada ya uchaguzi wa rais.

Mwezi uliopita Marekani ilisema inaondoa wanajeshi wake 100 kutoka Chad baada ya serikali kuhoji uhalali wa shughuli zao nchini humo.

*DW*

## Polisi wawatia mbaroni waandamanaji 63 Georgia

**TBILIS, Georgia**

WATU kadhaa wamekamatwa nchini Georgia, baada ya polisi kukabiliana na waandamanaji wanaopinga sheria inayokandamiza uhuru wa kujieleza.

Polisi walitumia mabomu ya machozi wakati maandamano yalipotokea katika mji mkuu wa Tbilis na kuwakamata watu 63.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Georgia, ilisema waliwakamata watu hao kwa makosa ya kushiriki maandamano haramu.

Mbuge wa upinzani, Levan Khabeishvili, alituma picha yake katika mtandao wa kijamii ikionyesha uso wake uliojaa damu kutokana na majeraha huku wanachama wa chama chake wakidai walishambuliwa na polisi.

Muswada huo unataka vyombo vya habari na mashirika ambayo sio ya kibiashara yanayopokea zaidi ya asilimia 20 ya ufadhili wao kutoka nje, yajisajili kwanza kama mashirika yanayofuatilia na kuendeleza maslahi ya nchi za kigeni.

*DW*

# NBC YAJIVUNIA KUCHOCHEA AJIRA KWA KUDHAMINI BARA

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani, ambayo kitaifa yamefanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki, Benki ya NBC imejivunia udhamini wake wa ligi tatu muhimu nchini ikiwamo Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ikiitaja hatua hiyo ni moja ya kichocheo muhimu katika kuongeza fursa za ajira kupitia michezo.

Pamoja na Ligi Kuu ya NBC, benki hiyo pia inadhamini Ligi Daraja la Kwanza (NBC Championship), Ligi ya Vijana (NBC Youth League) pamoja na kuandaa mbio za NBC Marathon ambazo hufanyika kila mwaka jijini Dodoma.

Akizungumza katika maadhimisho yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Mkurugenzi wa Idara ya wateja wadogo na Wakubwa wa NBC, Elibariki Masuke, alisema udhamini wa benki hiyo katika ligi hizo umechochea ongezeko la ajira kufuatia maboresho ya hali ya kiuchumi katika timu zinazoshiriki kupitia udhamini wao pamoja na wadau wengine.

"Katika maadhimisho haya NBC tunaungana na maelfu ya wafanyakazi wenzetu kote nchini kusheherekea siku hii muhimu sana kwa wafanyakazi, kwanza tukiwa kama wafanyakazi, pili tukiwa wadhamini muhimu katika kufanikisha uratibu wa maadhimisho haya, tatu tunashiriki kama watoa huduma za kifedha kwa wafanyakazi kupitia matawi yetu yaliyopo kote nchini na nne sisi tunachochea ajira kupitia michezo ambapo udhamini wetu katika ligi tatu muhimu hapa nchini umetoa fursa za ajira kwa mamia ya Watanzania," alisema.

Mbali na utoaji wa mikopo ya usafiri kwa timu zinazoshiriki ligi hiyo, Masuke alisema benki hiyo inaendelea kushirikiana kampuni washirika wa huduma za Bima kutoa huduma za bima za afya na maisha kwa wachezaji wote wanaocheza Ligi Kuu ya NBC, mabenchi ya ufundi pamoja na familia zao hatua ambayo inadhihirisha dhamira ya mdhamini huyo katika kujali afya na usalama wa wadau wa michezo, kitu ambacho ni muhimu kwa wafanyakazi.

"Wachezaji kama wafanyakazi wengine pia wanahitaji motisha pindi wanapofanya vizuri kwenye majukumu yao. Kwa kutambua hilo udhamini wetu katika Ligi Kuu ya NBC unahusisha utoaji wa zawadi za fedha taslimu na tuzo maalum kwa wachezaji na makocha wanaofanya vizuri kwenye ligi hiyo kila mwezi," Masuke aliongeza.

Alisema ili taifa liweze kufungua zaidi fursa za ajira kwa vijana ipo haja kwa serikali na wadau wengine kuwekeza zaidi katika sekta ya michezo kwa sababu ina uwezo wa kuajiri idadi kubwa ya watu hususani vijana.




Baadhi ya wafanyakazi wa benki ya NBC wakiwa katika maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), ambayo kitaifa mwaka huu yamefanyika jijini Arusha na yaliyoongozwa na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vita kushuka daraja yakolea

**Na Faustine Feliciane**

HUKU Ligi Kuu Tanzania Bara ikitarajiwa kuingia katika mzunguko wa 25, timu saba ziko kwenye vita ya kukwepa kushuka daraja.

Katika msimamo wa ligi mpaka kufikia leo, timu iliyoko kuanzia nafasi ya saba hadi ya 15 zimepishana kwa wastani wa pointi moja na kufanya mchuano wa kusaka nafasi yakubakia ligi kuu msimju ujao kuwa mkubwa.

Mtibwa Sugar inayoburuza mkia yenyewe ni kama imeweka mguu mmoja ligi ya championship kutokana na alama walizokusanya mpaka sasa.

Imecheza michezo 23 na kukusanya pointi 17 ikiwa imefungwa magoli 39 na kufunga magoli 23, timu ambayo ipo juu yake (nafasi ya 15), Tabora United yenyewe ina pointi 23 sawa na Geita inayoshika nafasi ya 14 kutokana na uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa kulinganisha na Tabora United huku timu zote zikiwa zimecheza michezo 24.

Geita Gold FC na Ihefu zenyewe zinashika nafasi ya 13 na 12 zikiwa zimepishana pointi moja tu na timu za Mshujaa na Tabora United na kufanya vita ya kushuka daraja kuwa kali kwa timu hizo kutokana na utofauti mdogo wa pointi baina yao.

„Ligi imekuwa ngumu, hatupo katika nafasi nzuri hata kidogo, lakini huwezi kusema tumeshuka, kuna utofauti mdogo wa pointi kwa timu za chini, hii ina maana kama tunataka kutoka tulipo lazima tuhakikishe hatudondoshi tena pointi," alisema Kocha wa Tabora United, Masoud Djuma.

## FettyDensa atamani kucheza soka Ulaya

**Na Somoe Ng'itu**

BEKI wa Simba Queens, Fatuma Issa ‚Fetty Densa' amesema bado ndoto yake ya kucheza soka nje ya Tanzania haijapotea na anaamini nafasi ya kusajiliwa na klabu za nje anayo.

Fetty Densa aliliambia gazeti hili anaendelea kujituma katika mazoezi na kuhakikisha anapata namba katika kikosi cha kwanza cha timu yake ambayo inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Beki huyo alisema ushindani wa namba kwa sasa ni mkubwa na kwake inamsaidia kuboresha kiwango chake kwa kupambana mazoezini na kwenye kila mechi anayopangwa.

„Bado nitaendelea kujituma kuhakikisha ninaisaidia timu yangu kufikia malengo, ligi ni ngumu na ushindani wa wachezaji unaongezeka, „ alisema beki huyo ambaye pia anaichezea Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars).

Nyota huyo ambaye alijiunga na Simba Queens akitokea Evergreen ya Temeke, Dar es Salaam aliwavutia Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini baada ya kuonyesha kiwango kizuri katika michuano ya Ligi ya Mabingwa ya Wanawake Afrika ya mwaka juzi, ingawa walitolewa katika hatua ya nusu fainali.

## KMKM yafunguka mechi zote ngumu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa KMKM SC, Ame Msimu amesema Ligi Kuu Zanzibar sasa imefikia katika hatua ‚ngumu' kutokana na kila mechi inayochezwa iwe nyumbani au ugenini kutokuwa rahisi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msimu, alisema ligi hiyo imeingia hatua ya lala salama ambayo kila timu inajipanga kufanya vizuri ili kufikia malengo.

Msimu alisema licha ya kupata alama tatu katika mechi yake ya mzunguko wa 21 iliyochezwa juzi, bado anakiri kikosi chake kina tatizo katika safu yake ya ulinzi.

„Safu yangu ya ulinzi ni tatizo, tunajitajidi kufanyia kazi kila baada ya mechi lakini bado naona hatujakuwa vyema, hivyo ni lazima nijue kiini cha tatizo, hatuhitaji kupoteza pointi katika," alisema Msimu ambaye timu yake ina pointi 42 na iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo, vinara ni JKU yenye pointi 44.

Kocha huyo aliongeza anaendelea kufanya maboresho ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi yake itakayochezwa leo dhidi ya Jamhuri ya Kisiwani Pemba ili kujiimarisha kwenye mbio za kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMUUZA JESUS

ARSENAL inajiandaa kupokea ofa kutoka katika timu mbalimbali ili kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Jesus, mwenye umri wa miaka 27 katika msimu wa majira ya joto (Athletic - ***subscription required)***

### ARSENAL NA JORGINHO

ARSENAL ina matumaini kiungo wa Timu ya Taifa ya Italia, Jorginho, mwenye umri wa miaka 32, atakataa ofa kutoka Juventus, Lazio na Napoli kwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Ligi Kuu England. ***(Standard)***

### EVERTON KUMUUZA PICKFORD

EVERTON italazimika kumuuza golikipa wa Timu ya Taifa ya England, Jordan Pickford (30), kama mpango wa mmiliki mpya wa klabu hiyo wa Kampuni ya 777 hautafanikiwa. (***Talksport)***

### ONANA AGOMBEWA ULAYA

ARSENAL, Bayern Munich na Newcastle United ni baadhi ya timu zinazovutiwa na kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji na Everton, Amadou Onana, 22. ***(Football Transfers)***

### FERNANDES AITEGA UNITED

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes (29), amesema hatima yake ndani ya kikosi cha Manchester United itatokana na uamuzi utakaofanywa na mabosi wa timu hiyo katika kipindi cha msimu wa joto. ***(Telegraph - subscription required)***

### TONEY KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney na wanaamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ataleta uzoefu na uongozi katika kikosi chao. ***(90min)***

### SPURS YAMTAKA TONEY

TOTTENHAM Hotspur nayo imeonyesha nia ya kujitosa kumwania, Ivan Toney kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(GivemeSport)***

### UNITED KUTEMA NYOTA 12

KLABU ya Manchester United inalenga kuwaachia wachezaji 12 msimu huu wa joto, akiwamo fowadi wa Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 26, na kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro (32). ***(Mirror)***

### POCHETTINO MAMBO MAGUMU

MUSTAKABALI wa Mauricio Pochettino kama kocha wa Chelsea upo katika mizani na unaweza kutegemea iwapo anaweza kufuzu kwa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.***(Times)***


### OSIMHEN AKARIBIA PSG

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25 anakaribia kujiunga na Paris Saint-Germain ya Ufaransa, lakini mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Nigeria pia ameivutia Chelsea. ***(Il Mattino)***

### DIOMANDE ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa kati wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 20, Ousmane Diomande, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 80. ***(A Bola)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA AREJEA MADRID KUTIBIWA

Ni baada ya kukumbwa na majeraha ya mara kwa mara tangu...

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wanamsaidia mchezaji wao wa zamani, Karim Benzema, kupona jeraha la mara kwa mara, klabu yake ya Al Ittihad ilithibitisha.

Benzema mwenye umri wa miaka 36, amekuwa na matatizo ya misuli katika msimu wake wa kwanza akiwa na klabu hiyo inayoshiriki Saudi Pro League aliyojiunga nayo msimu uliopita wa kiangazi akiwa mchezaji huru baada ya miaka 14 ya kuitumikia Real Madrid.

Fowadi huyo alicheza kwa mara ya mwisho katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Al Hazm mnamo Aprili 20, mwaka na amekosa michezo miwili iliyopita.

„Karim Benzema anafanyiwa uchunguzi zaidi katika kliniki ya Real Madrid na daktari wake wa zamani wa nchini Hispania, ambaye alimsimamia miaka ya nyuma,“ Al Ittihad ilisema katika taarifa yake.

„Mashauriano yalipangwa kati ya timu za matibabu za Ittihad na Real Madrid kuhusu majeraha ya Benzema, ambayo yalimfanya kukosa mechi muhimu msimu huu. Benzema tayari ameondoka kuelekea Hispania na anatarajiwa kurejea wiki ijayo.“

Benzema amefunga mabao 13 katika mechi 29 katika michuano yote akiwa na klabu hiyo yenye maskani yake Jeddah.

Mshindi hugo wa Ballon d'Or 2022 ana mkataba na Al Ittihad hadi Juni, mwaka 2026.

# FERNANDES AFIKIRIA HATIMA YAKE UNITED

**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes amesema atafikiria mustakabali wake ndani ya Manchester United baada ya michuano ya Ulaya msimu huu akiwa na Ureno.

Nahodha huyo wa United amesisitiza anaangazia kikamilifu Fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City itakayochezwa Mei 25, mwaka huu na kushiriki michuano ya Euro huko Ujerumani.

Huku kukiwa na tetesi za vyombo vya habari anaweza kuondoka United, alipoulizwa kuhusu mustakabali wake, Fernandes mwenye umri wa miaka 29, aliiambia Dazn Ureno: "Sina mawazo ya mambo mengine kwa sasa."

"Kwa hiyo, kama unataka niwe mkweli, ikibidi nifikirie kutoendelea kwenye Ligi Kuu, haitakuwa hadi baada ya Euro.

"Tunaweza kumaliza msimu kwa kutwaa Kombe la FA, halafu tunakuwa na Ubingwa wa Ulaya, ambao ni muhimu sana kwetu.

"Hakuna kitakachoondoa umakini wangu kutoka mwisho huu wa ubingwa, Kombe la FA na Ubingwa wa Ulaya. Hakuna kitu muhimu zaidi kuliko hicho kwa sasa."

Fernandes, ambaye yuko katika msimu wake wa tano na United, alisema anahisi kuhitajika Old Trafford.

"Mchezaji siku zote lazima atake kuwa hapa, lakini wakati huo huo, lazima utake abaki. Kwa sasa, ninahisi kuna hiyo pande zote mbili," Fernandes alisema.



"Sifikirii sana juu ya siku zijazo, hata kidogo kwa sababu, ni wazi, msimu huu haujawa katika kiwango nilichotarajia, kibinafsi au kwa pamoja, hadi sasa."

Mnamo Machi, mwaka huu, Fernandes alisema alikutana na wamiliki wapya wa United na kuwaambia anataka kubaki katika kilabu hicho, ambapo ana mkataba hadi Juni 2026.

Hata hivyo, aliongeza: "Nataka kuwa mshindani, nataka kushindana, nataka kushinda."

Fernandes ametwaa taji moja pekee, Kombe la Carabao msimu uliopita, tangu ajiunge na United kutoka Sporting CP Januari, mwaka 2020 kwa mkataba wa thamani ya hadi Euro milioni 80.

Amefunga mabao 15 na kutengeneza mengine 11 katika mechi 45 alizoichezea United msimu huu.

## Araujo bado atakiwa Barca

**BARCELONA, Hispania**

BEKI wa Barcelona, Ronald Araujo, anadaiwa kutathmini kile kinachotajwa kuwa "ofa ya mwisho" juu ya mkataba mpya ambayo inaonekana kuamua hatua inayofuata ya maisha yake ya soka.

Mkataba wa sasa wa Araujo utaendelea hadi 2026 na uvumi kuhusu mustakabali wake umekuwa mwingi katika miezi ya hivi karibuni huku akidawaia kutakiwa Bayern Munich na Manchester United haswa.

Dail Mail imeandika Barcelona inamtaka beki huyo wa kati wa Uruguay, aliyepandishwa katika kundi la manahodha wa kikosi hicho msimu huu, aendelee kwa kusaini mkataba mipya.

Yeye pia anasemekana kupendelea kujitolea kwa mkataba mpya lakini bado hajatoa jibu na chaguzi zingine zinaonekana kuwa wazi.

Mkataba uliopendekezwa wa miaka minne Camp Nou hadi 2028 unaripotiwa kujumuisha nyongeza ya mshahara, ingawa hautamweka Araujo miongoni mwa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi kikosini, licha ya hadhi yake ya juu.


Kuwasilisha ofa ambayo inaweza kuchukuliwa "haiwezekani" kwa sababu ya viwango vya juu vya mishahara vilivyopo na kuna "nafasi ndogo sana ya kuboresha" namba zilizo katika jedwali kwa sasa.

Uamuzi wa mwisho utakuwa wa mchezaji huyo, lakini Barcelona watafaidika ikiwa wataamua kutoongeza muda kwa sababu ya fedha ambazo mauzo ya msimu wa joto yanaweza kuleta kuongeza bajeti.

Bayern Munich wameripotiwa kumtaka na Manchester United wameifahamisha kambi ya mchezaji huyo watatoa ofa rasmi iwapo kutakuwa na nia ya kuondoka Barcelona.

Bayern Munich wanaweza hata kuishia katika nafasi nzuri kwa sababu ya Barcelona kumtaka Joshua Kimmich na uwezekano wa Araujo kujumuishwa katika mazungumzo yoyote ambayo yanaweza kuanza.

Iwapo Araujo hatatia saini mkataba na kuingia miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake wa sasa, Barcelona wana hatari ya kupoteza kifedha ikiwa hawatajaribu kupata fedha kabla ya thamani yake sokoni kuanza kushuka.



## Arsenal kumweka sokoni Jesus

**LONDON, England**

ARSENAL iko tayari kusikiliza ofa za kumnunua mshambuliaji Gabriel Jesus katika dirisha lijalo la usajili la majira ya kiangazi, kwa mujibu wa ripoti.

Washika bunduki hao walimnasa fowadi huyo wa Brazil kutoka Manchester City mwaka 2022 na alionesha kuwasili kwa mageuzi katika msimu wake wa kwanza kwenye Uwanja wa Emirates kabla ya kupata jeraha la goti ambalo lilimfanya akose mechi nyingi.

Hata hivyo, ingawa amelazimika kushinda jeraha la hapa na pale hadi sasa 2023/24, Jesus amefunga mabao manne pekee ya Ligi Kuu ikilinganishwa na 11 msimu uliopita na amekuwa nyuma ya Kai Havertz aliyecheza vizuri kwa kiwango kikubwa chini ya kocha Mikel Arteta.

The Athletic sasa linadai kwamba, licha ya fowadi huyo mwenye umri wa miaka 27 kubakiwa na miaka mitatu katika mkataba wake wa sasa, Arsenal watasikiliza ofa nzuri kumuuza mchezaji Hugo.

Amekuwa akisumbuliwa na jeraha la goti tangu Kombe la Dunia la 2022, akifichua mapema Aprili: "Sikumbuki mara ya mwisho nilicheza soka bila maumivu. Ninajaribu kuweka nguvu akilini."

Nafasi yake ya kurejea katika kikosi cha kwanza imepunguzwa na uchezaji mzuri wa Havertz.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani anaonekana kuwa sawa mbele ya Arsenal na alifikisha hadi mabao 12 ya ligi msimu huu wakati wa ushindi wa 3-2 wa dabi ya London kaskazini dhidi ya Tottenham Hotspur Jumapili.

Jesus hakutumika kama mchezaji wa akiba katika ushindi huo ambao ulilinda uongozi wa wa Arsenal kileleni mwa jedwali la Ligi Kuu.



HABARI MICHEZO

# MAJALIWA MGENI BETIKA TULIA MBEYA MARATHON

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI hamasa ya kushiriki ikiwa imeongezeka, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika mbio ya Betika Mbeya Tulia Marathon zitakazofanyika Mei 10 na 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

Ofisa habari wa Taasisi ya Tulia Trust, Joshua Edward, alisema jijini Dar es Salaam jana, maandalizi ya mbio hizo yamekamilika na Waziri Mkuu Majaliwa atakuwa na mwenyeji wake, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Joshua alisema wanatarajia wanariadha zaidi ya 5,000 kutoka mikoa mbalimbali nchini watashiriki mbio za mwaka huu na baadhi ya mikoa imeanza 'amsha amsha' ikiwamo Mtwara ambao jana wadau wameshiriki mbio iliyoratibiwa na radio ya Newala FM zikiongozwa na Meya wa Manispaa ya Newala, Hamis Namata.

Meya huyo aliwakabidhi washiriki watano bendera ya Tulia Marathoni na Betika tayari kuipeperusha watakapokwenda Mbeya.

Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvelinaus, alisema wanariadha hao watalipiwa gharama zao zote na kampuni yao.

"Watu watano waliokimbia leo (jana) watagharamiwa na Betika watakapokuwa katika mbio za Betika Mbeya Tulia Marathoni," alisema Rugambwa.

Aliitaja mikoa mingine ambayo itafanya mbio 'ndogo' ili kuwaweka tayari washiriki wake ni pamoja na Dodoma, Iringa, Rukwa na Morogoro.

Alisema mbali na hao wa Mtwara, Betika pia itawagharamia wanariadha wengine 420 kutoka mkoa mwenyeji wa Mbeya na washiriki wengine 10 kutoka Dodoma, Iringa, Morogoro na Rukwa.




Meya wa Manispaa ya Newala, Hamisi Namata (watatu kushoto), akiwakabidhi bendera ya Betika washindi watano ambao wataiwakilisha Mtwara katika mbio za mwaka huu za Betika Mbeya Tulia Marathon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fei Toto kinara mabao ndani ya boksi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', ndiye kinara wa kufunga mabao ndani ya eneo la hatari mpaka kufikia raundi ya 24 ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

Takwimu za dawati la michezo la Nipashe pamoja na Bodi ya Ligi zilizotolewa jana, Fei Toto amefunga mabao 13 akiwa katika eneo la 18.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea Yanga, ana mabao 14 ya kufunga mpaka sasa, hivyo takwimu zinaonyesha ni bao moja tu alilolifunga akiwa nje ya boksi.

Wanaoshika nafasi ya pili kwa kupachika mabao ndani ya boski ni kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki na straika wa KMC, Waziri Junior, ambao wote wamefunga magoli 10 wakiwa ndani ya eneo la hatari.

Aziz Ki, ndiye kinara wa ufungaji kwenye ligi mpaka sasa, akiwa na mabao 15, hivyo mabao matano ametafunga akiwa nje ya eneo la hatari na Waziri ana mabao 11, hivyo ni bao moja tu ambalo amelifunga akiwa mbali na lango.

Takwimu zinaonyesha kiungo mwingine wa Yanga, Mkongomani Maxi Nzengeli na straika wa Prisons, Samson Mbangula, wamefunga mabao manane ndani ya boksi kila mmmoja.

Nzengeli amefunga tisa katika Ligi Kuu, hivyo moja amelifunga nje ya boksi, lakini Mbangula ana mabao manane, mabao yote aliyoyafunga, ameyapachika akiwa ndani ya eneo la hatari.

Wachezaji Jean Baleke aliyekuwa akichezea Simba, Prince Dube wa Azam FC, Pacome Zouzoua na Mudathir Yahya wa Yanga, wote wana mabao saba kila mmoja waliyoyafunga wakiwa ndani ya eneo la hatari.

Takwimu zinaonyesha Baleke na Mudathir ambao kila mmoja ana mabao manane, kila mmoja kati yao amefunga bao moja nje ya boksi, lakini Dube na Pacome mabao yao yote saba wameyapachika wakiwa ndani ya eneo la hatari.

## Manula, Kibu watakiwa Azam

INATOKA UK. 24

Vijana wapo vizuri na wanajua uzito wa mechi hii na umuhimu wake, wachezaji wapo tayari kwa mchezo kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kwa kuvuna pointi tatu muhimu,"alisema Mgunda.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani kwa sababu wanakutana na Simba ambayo imetoka kugawana pointi na Namungo na leo wanahitaji kupata matokeo chanya.

Katwila alisema wamefanyia kazi na kusahihisha mapungufu yao na sasa wanaenda kukutana na wapinzani kwa tahadhari kubwa.

"Unapochsza na Simba haijalishi wanakosa wachezaji gani, hata sisi tunakosa baadhi ya wachezaji lakini tumejipanga, tuna presha ya kutafuta matokeo mazuri kama ilivyo kwa wapinzani wetu," alisema Katwila.

Katika hatua nyingine Azam inashuka dimbani kuikaribisha Namungo FC katika mchezo wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo.

"Tutaona namna gani ya mabadiliko na kuingia vipi katika mchezo huo ili kutafuta ushindi na kwenda kucheza nusu fainali, Namungo ni timu ngumu kucheza nao, tunatakiwa kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa ajili ya kupambania kombe hili," alisema, Kocha Msaidizi wa Azam, Bruno Ferry.

## Guede afunguka anataka mabao 17

INATOKA UK. 24

wake na kila anachokitoa kwa ajili ya timu," alisema Gamondi.

Kocha huyo aliongeza anaamini Guede ataendelea kufanya vizuri na anajivunia uwezo wa wachezaji wake lakini pia akifurahia kurejea kwa, Pacome Zouazou.

„Nimefurahi sana kuingia nusu fainali, lakini sifa ni kwa wachezaji, tuna muda mchache kutoka mchezo mmoja na mchezo mwingine lakini wachezaji wangu hilo hawalijali, wanapambana uwanjani na hii ndio faida yake, nawapongeza sana," alisema Gamondi.

Aliongeza kurejea kwa nyota wake, Pacome ni jambo zuri kwake na anaamini hata mashabiki wa timu hiyo wamefurahi kumwona tena uwanjani.

„Upana wa kikosi changu unaongezeka kwa kurejea kwa Pacome, ni jambo uzri na nimefurahi, nimeanza kwa kumpa dakika 25 ili taratibu arejee kwenye utimamu wa mechi, nitakuwa nikimwongezea dakika taratibu mpaka arudi katika hali yake kiuchezaji, naamini na mashabiki wamefurahi kumwona akirejea uwanjani," alisema Gamondi.

Yanga wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 62 baada ya kucheza michezo 24 ikifuatiwa na Azam wakati Simba wanashika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 15 pungufu ingawa wamecheza michezo 22.

**Michezo**

Ijumaa Mei 3, 2024

**Nipashe**

## Benzema arejea Madrid kutibiwa

UKURASA 21







# MANULA, KIBU WATAKIWA AZAM

## ●●●Matajiri hao watenga dau nono kuwang'oa, Simba, Mtibwa kibaruani...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba inatarajia kuikaribisha Mtibwa Sugar katika mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara, nyota wake, Aishi Manula na Kibu Denis, wanatajwa kuwindwa na Azam FC ambayo imedhamiria kujiimarisha kwa ajili ya kufanya vizuri katika msimu ujao.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinasema Azam inadaiwa kutenga dau la Sh. milioni 300 na kumpa mkataba wa miaka miwili Kibu, ikipanga kumlipa Sh. milioni 150 kwa mwaka.

Chanzo chetu kilisema matajiri hao wa Chamazi pia wameweka dau nono la kuhakikisha Manula anarejea katika timu yake ya zamani kwa sababu wanaamini nyota huyo mwenye uzoefu atawasaidia kufikia malengo katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Chanzo hicho kilisema Azam ilipiga hodi Msimbazi baada ya kubaini mkataba wa Kibu umebakiza miezi sita sawa na Manula ambaye kwa sasa ni majeruhi.

„Ni kweli tunahitaji kuimarisha timu yetu na kulingana na mahitaji tuliyonayo ni pamoja na kuimarisha safu ya ushambuliaji na eneo la kipa, na hapo wanatajwa Kibu na Manula. Ofa zao zipo mezani na mambo yakienda vizuri msimu ujao watakuwa mali ya yetu," kilisema chanzo chetu.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema wako katika mchakato wa kuboresha timu yao katika kila eneo lenye uhitaji.

Popat alisema wanahitaji kufikia malengo na watafika huko kwa kuhakikisha wanasajili wachezaji wenye ubora na uzoefu.

Alisema baada ya kufanikiwa kumnasa nyota, Frank Tiesse, kutoka katika Klabu ya Stade Malien ya Mali, sasa wako katika mchakato wa kukamilisha usajili wa nyota wengine wawili wazawa.

„Ni kweli sasa akili na nguvu zetu ni katika kujiimarisha, kwa sasa tunataka kukamilisha mchakato wa wachezaji wawili ambao ni raia wa hapa Tanzania. Ni wachezaji ambao watakiongezea nguvu kikosi chetu," Popat alisema.

Kuelekea mechi dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kuanzia saa 10:00 jioni, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema hii ni ligi na hawawezi kuwajadili wapinzani wao na wataingia kwa tahadhari katika mechi hiyo.

Mgunda alisema licha ya kutokuwa na matokeo mazuri, Mtibwa Sugar ni timu ngumu na wamejiandaa vyema kuwakabili.

„Tutamkosa Chama (Clatous), katika mchezo wa kesho (leo) kutokana na adhabu aliyoipata, lakini Simba imefanya usajili wa wachezaji wengi na watapata nafasi ya kucheza na kuonyesha kitu kizuri.

INAENDELEA UK. 23

# Guede afunguka anataka mabao 17

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kufunga bao moja katika ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Tabora United katika mchezo wa robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA, mshambuliaji wa Yanga, Joseph Guede, amesema atahakikisha anafunga mabao 17 kwenye michuano yote msimu huu.

Guede ambaye alianza kwa kusuasua baada ya kujiunga na Yanga, kwa sasa amekuwa ,moto', akifunga mabao muhimu kwa timu yake katika mashindano mbalimbali yanayoendelea.

Bao alilofunga nyota huyo raia wa Ivory Coast katika mchezo wa juzi dhidi ya Tabora United, limemfanya afikishe mabao nane katika mashindao yote mpaka sasa.

„Nafurahia kuifungia timu yangu, nataka niwe nafanya hivi katika kila mechi ninayopata nafasi ya kucheza, malengo yangu ni kufunga angalau mabao 17 msimu huu," alisema Guede.

Mshambuliaji huyo alisema ataendelea kushirikiana na wachezaji wenzake kuhakikisha Yanga inafikia malengo yake msimu huu kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu pamoja na kutetea Kombe la FA.

„Nadhani bado tupo katika malengo yetu kama klabu na hilo ndio la muhimu, kikubwa ni kuhakikisha tunafikia malengo yetu msimu huu," alisema Guede.



Kuhusu kiwango cha mshambuliaji huyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema anafurahishwa na jitihada na uwezo wa nyota wake huyo.

„Amekuwa na kiwango kizuri, anatufungia kila mechi, nafurahishwa na uwezo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >